# Nipashe

Jumatano Oktoba 7, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580361

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


**Washikiliwa** kwa madai ya kuingilia mitandao ya kibenki

UKURASA 3



**Polisi** wamzuia Lissu kufungua matawi Kibaha

UKURASA 2




**Rafinha wa Barca ajiunga na PSG**

UKURASA 21

# Mgombea ubunge apata mkong'oto

• **Adaiwa** kuvamia uwanja wa CCM, kupiga muziki wa kampeni, mwenyewe ajitetea... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**RAIS WA MALAWI KUJA NCHINI LEO**

RAIS wa Malawi, Lazarus Chikwera, anatarajia kuwasili nchini leo kwa ziara ya siku tatu, ambayo pamoja na...

## Uswisi yaipatia Tanzania bilioni 44/-

UKURASA 3



Baadhi ya wanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Themi, jijini Arusha, wakisafisha madawati, shuleni hapo jana, kwa ajili ya maandalizi ya mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi, inayoanza leo. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




# TLP, UDP zajiondoa kumpigia debe JPM

UKURASA 2


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

VOTE

# TLP, UDP zajiondoa kumpigia debe mgombea urais CCM

**Na Thobias Mwanakatwe**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini imesema vyama vya Tanzania Labour (TLP) na United Democratic (UDP) ambavyo vilitangaza kumuunga mkono mgombea urais wa Tanzania kupitia CCM, John Magufuli, vilisitisha mpango huo kwa sababu vilikuwa havijafuata kanuni na sheria za uchaguzi.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sity Nyahoza, alisema hayo jana wakati akihojiwa na Radio One kwenye kipindi cha Kumepambazuka.

Mapema mwaka huu, Mwenyekiti wa Taifa wa TLP, Augustino Mrema, na Mwenyekiti wa UDP, John Cheyo, kwa nyakati tofauti, walitangaza kuwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, vyama vyao havitaweka wagombea urais badala yake vitamuunga mkono mgombea wa CCM.

Hata hivyo, Nyahoza jana alisema katika uchaguzi wa mwaka huu, viko vyama ambavyo vilishawahi kupewa onyo na vikarekebishika.

"Mfano kuna Chama cha UDP na TLP walitangazaga kwamba wanamuunga mkono mgombea wa CCM, tukawaambia kuna utaratibu wake, hivyo hamjafuata inabidi mfuate. Wakaona hawajafuata utaratibu ikabidi wakae kimya, sasa hivi unawasikia tena?" Alihoji.

Alisema hivi sasa UDP baada ya kuelezwa walielewa na wanaendelea na kazi zao za kampeni na wana wagombea wao ambao wanaendelea kutangaza sera za chama chao.

Nyahoza alisema TLP kwa upande wake kiliweka hadi na bango na baada ya kuelezwa hakijafuata utaratibu, kiliyatoa sasa wanaendelea na kampeni zao.

"Kwa hiyo vyama ni sikivu, vile ambavyo siyo sikivu wawe wasikivu na kuzingatia sheria na kanuni maana kama mgombea wa chama chako msipokuwa wasikivu ukishinda kwenye uchaguzi itakuwaje," alisema.

Aidha, Nyahoza alisema vyama lazima vitambue kuwa kama huna amani na utulivu huwezi kuwa na uchaguzi.

"Unapokaa jukwaani ukaongea ukanadi sera yako au hata ukaongea mambo yako yawe ya ovyo au ya msingi ujuwe unaongea sababu kuna amani, huwezi kwenda kukaa sehemu risasi zinapigwa, vurugu watu wanafukuzana utapataje muda wa kukaa," alisema.

Aliongeza kuwa msajili wa vyama vya siasa ambaye kisheria ndiye msimamizi na mlezi wa vyama vyote vya siasa, ataendelea kuvishauri na kuvionya vile ambavyo vinakiuka sheria na kanuni.

"Msajili ni mlezi wa vyama vya siasa hivyo inapotokea mtu amekiuka sheria taratibu kwenye kampeni wajibu wake kama mlezi ni kumuonya kwamba unachofanya siyo sahihi, akiendelea kufanya unamuonya tena si unajua mambo ya ulezi tena na ndiyo maana unaona tunawaandikiaga barua sana vyama vya siasa vile ambavyo vinakiuka taratibu na sheria," alisema.




Mgombea ubunge wa Jimbo la Ubungo kupitia CCM, Prof. Kitila Mkumbo, akikwea daladala wakati akiwa kwenye harakati za kuomba kura kwa wananchi wa jimbo hilo, katika eneo la Shekilango, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi wamzuia Lissu kufungua matawi

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani, limesema kuwa limemzuia Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, eneo la Kiluvya, kuzungumza na wananchi kwa maelezo kuwa hiyo ni sehemu ya kampeni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, aliiambia Nipashe jana kuwa:

"Ni kweli tumemzuia kuanzia saa 5 asubuhi, baada ya kupata taarifa jana (juzi) kwamba Mheshimiwa Tundu Lissu atakuwa na shughuli ya kutembelea soko la Mlandizi na baadaye atazindua matawi mbalimbali ya chama chake.

Wakati tunafuatilia taarifa hizo tukakuta watu kuanzia saa 3 wanafanya maandalizi ya kumpokea leo tarehe 6 (jana)."

Kamanda Nyigesa alisema kitendo cha kuongea na wananchi pamoja na kutembelea soko kinaonyesha ni kufanya kampeni na amezuiwa.

"Akisema anafungua matawi ya chama ni shughuli za kisiasa ambazo Jeshi la Polisi linatakiwa kupewa taarifa, na hajatoa taarifa kwetu, maana yake amekiuka sheria, sisi tuna ushahidi sio mikutano ya ndani," alisema Kamanda Nyigesa.

Aidha, Kamanda alisema Lissu hashikiliwi na Polisi, ingawa tangu majira ya asubuhi alikuwa eneo hilo.

Awali katika mitandao ya kijamii na katika ukurasa wa twitter wa Lissu, aliandika kwamba msafara wake umezuiwa maeneo ya Kiluvya Gogoni, akielekea Kibaha Mkoa wa Pwani.

"Tulikuwa tunaenda kutembelea soko na kufungua matawi si kampeni, ila Jeshi la Polisi limetuzuia, aliandika Lissu kwenye ukurasa huo na kuongeza;

"Nilikuwa na ratiba ya kufanya kikao cha ndani ya chama hapa Kibaha, nimeambiwa nimezuliwa kufanya kampeni na kutakiwa kubaki Dar, lakini vikao vya ndani sijazuiliwa kufanya."

Lissu mgombea urais kupitia CHADEMA, alisimamishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kufanya kampeni kwa siku saba baada ya kukutwa na hatia ya kukiuka maadili ya uchaguzi.

NEC kupitia mkurugenzi wake wa huduma za sheria, Emmanuel Kawishe, alisaini waraka wa kumsimamisha Lissu kufanya kampeni zake kwa muda huo na kueleza kwamba, Lissu anayo nafasi ya kukata rufani dhidi ya uamuzi huo.

# Mgombea NCCR-Mageuzi apata mkong'oto

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Bariadi, mkoani Simiyu kupitia Chama cha NCCR-Mageuzi, Askofu Erasmus Lilanga na wasaidizi wake wawili jana walishambuliwa na kusababishiwa majeraha mwilini baada ya kuingia eneo la uwanja wa CCM na kupiga muziki wa kampeni.

Akizungumza na waandishi wa habari jana nje ya hospitali ya Halmashuari ya Mji wa Bariadi (Somanda), alipokuwa akipatiwa matibabu, mgombea huyo alisema walivamiwa na vijana aliodai ni wa CCM wakati wakiwa kwenye harakati za mkutano wa kampeni.

Alisema kuwa katika uvamizi huo, gari lake aina ya Noah lilivunjwa vioo vya mbele na mlangoni, huku mmoja wa wasaidizi wake akiumizwa kichwani kwa kupigwa na nondo.

Hata hivyo, maelezo ya mgombea huyo yalikinzana na maelezo yaliyotolewa na Kamanda wa Polisi mkoani humo, Richard Abwao juu ya chanzo cha tukio hilo.

Kamanda Abwao akizungumzia tukio hilo kwa waandishi wa habari, alisema kuwa mgombea huyo akiwa na gari lenye usajili namba T866 aina ya Noah pamoja na wasaidizi wake walivamia eneo walipokuwa vijana wa CCM ambao walikuwa wanaendelea na kikao.

Taarifa hiyo ya polisi ilisema kuwa mgombea huyo alifika kwenye uwanja wa CCM Bariadi ambako kuna Ofisi za wilaya, na kuanza kupiga muziki wa chama chake na kutoa matangazo ya kuhamasisha wananchi wahudhuria mkutano wake.

Kamanda Abwao alisema kuwa kitendo hicho kiliwachukiza vijana hao wa CCM na kilionekana kama usumbufu kwa kuwa walikuwa na kikao na kuamua kutoka ndani na kumtaka mgombea huyo kuondoka eneo hilo.

"Walimueleza aondoke kwani anawapigia kelele na siyo eneo lake bali ni eneo la CCM, huyo mgombea aliondoka, lakini baadaye alirudi akipiga mziki na matangazo kama mwanzo, ndipo zikatokea vurugu hizo," alisema Abwao.

Mgombea huyo akizungumza na waandishi wa habari, alisema kuwa yeye alikuwa anatafuta eneo ambalo amepangiwa kufanya mkutano wa kampeni na wasaidizi wake kwa kuwa siyo mwenyeji wa maeneo ya mji wa Bariadi.

"Mimi sikujua kama lile ni eneo la CCM, nilikuwa napita kuelekea kwenye mkutano wangu, ndipo vijana hao walifika na kuanza kutushambulia, na tuliwaeleza kuwa sisi tunatafuta uwanja ambako kuna mkutano wetu, lakini hawakutuelewa," alisema Lilanga.

Alisema kuwa kijana wake mmoja aliyeumizwa Gulya Juma, alikimbizwa hospitali na hali yake inaendelea vizuri, huku yeye akiwa ameumizwa jicho pamoja na eneo la kifua.

## HABARI KITAIFA

# Mbaroni madai kuingilia mitandao ya benki

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

MAKADA watano wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Arusha, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuingilia mifumo ya mawasiliano ya kibenki.

Vilevile, wanatuhumiwa kuendesha mafunzo batili yanayolenga kutenda uhalifu wa kijinai katika kipindi cha kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Salum Hamduni, alithibitisha jeshi hilo linawashikilia watu hao baada ya kuwakamata Oktoba 5 mwaka huu majira ya saa 11:45 jioni.

"Polisi ilipokea taarifa kuwapo kwa watu hao kwenye ofisi binafsi za aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini (Godbless Lema) zilizoko Mtaa wa Esso, ambako kumekuwa na kawaida ya watu kukusanyika kuendesha mafunzo ya kulenga kutenda uhalifu wa kijinai unaohusishwa na kuingilia mifumo ya mawasiliano ya kibenki.

"Sasa, baada ya taarifa hizo kupokewa, wapelelezi walifika eneo hilo kufanya uchunguzi. Askari wapepelezi walikwenda kwa nia ya kufanya upekuzi kwenye ofisi hizo na kukamata watu wote.

Kwa mujibu wa Kamanda Hamduni, waliokamatwa ni mdogo wake na Lema aitwaye Nelson Lema (31), mkazi wa Arusha ambaye ni mfanyabiashara.

Wengine ni Lazaro Viola (46), ambaye Katibu wa CHADEMA Wilaya ya Arusha, mfanyabiashara Wilbad Tarimo, Joshua Lukumay, mfanyabiashara na Mohamed Omar (45) ambaye ni wakala wa mabasi. Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi kuhusiana na taarifa hizo na inakusudia kuchukua hatua nyingine za kisheria kwa kadri ambavyo ushahidi utapatikana.

Katika taarifa yake, Kamanda Hamduni, alisema taratibu za dhamana kwa watuhumiwa hao ziko wazi na zinaendelea kushughulikiwa, hivyo taratibu zikikamilika watapewa haki hiyo.

Alisema Jeshi la Polisi halijihusishi na siasa na kwamba wajibu wa jeshi hilo umeelezwa kwenye katiba.

**KAULI YA LEMA**

Akizungumzia tukio hilo katika mkutano wake na waandishi wa habari jana jijini hapa, mgombea ubunge wa Arusha Mjini ambaye ni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Lema, alilaani kitendo akidai kuwa ni kinyume cha sheria.

Alisema askari polisi zaidi ya 30 walifika katika ofisi hizo huku wakiwa wamebeba silaha za moto na kufanya upekuzi kwenye ofisi hizo kwa zaidi ya saa tatu.

Kwa mujibu wa Lema, askari polisi hao walidai kuwa ofisini huko kulikuwa na wahamiaji haramu kutoka mataifa ya Kenya na Israel.

Lema alidai kuwa vitu vilivyochukuliwa na polisi ni pamoja na nyaraka za siri za chama, simu nane na kompyuta mpakato mbili.

Lema alisema: "Juzi majira ya saa 6:30 jioni, nilipokea taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa CHADEMA Arusha Mjini, kwamba maofisa wa Jeshi la Polisi walifika katika ngome hiyo na kuwakamata viongozi watano wa chama na kuchukua baadhi ya vifaa na nyaraka.

Alisema kuwa kutokana na polisi kuwakosa wahalifu waliodai kuwa wapo kwenye ofisi hizo, walibadilisha maelezo na kusema kuwa watu hao walikuwa kwenye mpango wa kuingilia mifumo ya kibenki kwa ajili ya kujipatia fedha za kuendesha uchaguzi.

***Imeandikwa na Allan Isack na Daniel Sabuni**

## Rais Malawi kuja nchini leo

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Malawi, Lazarus Chikwera, anatarajia kuwasili nchini leo kwa ziara ya siku tatu, ambayo pamoja na mambo mengine, atatembelea Bandari ya Dar es Salaam.

Pia akiwa na mwenyeji wake, Rais John Magufuli, wataweka jiwe la msingi katika ujenzi wa kituo cha kisasa cha mabasi Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kikanda, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema hiyo ni ziara yake ya kwanza ya kikazi tangu Rais huyo aingie madarakani mwezi Juni mwaka huu.

"Lengo la ziara yake ya kutembelea Tanzania kwa mwaliko wa Rais Magufuli, ni kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya nchi hizo mbili na kuendelea kudumisha ujirani mwema," alisema.

Alisema wakiwa bandarini pamoja na mambo mengine, watatembelea kituo cha kuhifadhia mizigo cha Malawi kilichopo hapo ambacho kimekuwa alama muhimu katika ushirikiano kati ya nchi hizo mbili.

Prof. Kabudi alisema uhusiano kati ya nchi hizo ni mzuri na zimeendelea kushirikiana katika nyanja ya kisiasa, ulinzi na usalama, kiuchumi na kijamii na mambo ya kikanda.

Alisema zimeshirikiana katika miradi ya pamoja ikiwamo ujenzi wa kituo cha kutoa huduma cha pamoja mpakani na kuboresha miundombinu katika ushoroba wa Mtwara.




Mgombea mwenza wa kiti cha rais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, akizindua tawi la chama hicho, katika Kijiji cha Msambiati, kabla ya kuhutubia mkutano wa kampeni katika Jimbo la Mtwara Vijijini jana. **PICHA: FRANCIS DANDE**

# Uswisi yaipatia Tanzania bil. 44/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI ya Tanzania imesaini mikataba miwili na Serikali ya Uswisi yenye thamani ya Sh. bilioni 44.1 kwa ajili ya kugharamia miradi miwili ya awamu ya pili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) na Mfuko wa Pamoja wa Afya.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kusaini mikataba hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema mkataba wa kwanza wenye thamani ya Sh. bilioni 39.15 ni kwa ajili ya mpango wa kaya maskini chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kuanzia mwaka 2020 hadi 2023.

"Mkataba wa pili ni marekebisho ya mkataba wa msaada wa Sh. bilioni 4.95 kwa ajili ya kuchangia mfuko wa pamoja wa afya kwa mwaka wa fedha 2020/21," alisema.

Alifafanua kuwa mkataba wa kwanza unalenga kuboresha upatikanaji wa fursa ya kujipatia kipato na huduma za kijamii kwa kaya maskini, kulinda na kuboresha nguvu kazi ya watoto wao kwa kulenga matokeo.

Alisema matokeo yanayolengwa ni kupunguza umaskini na kuboresha nguvu kazi, upatikanaji wa fursa za kujipatia kipato kwa kaya maskini na kujenga na kukinga nguvu kazi ya watoto, kuboresha uwezo wa kununua mahitaji ya kaya maskini na ushiriki wa kaya bora kwa ajili ya kujipatia kipato.

Alifafanua kuwa mpango wa kunusuru kaya maskini awamu ya kwanza ulitekelezwa kwa kipindi cha kwanza mwaka 2013 hadi Desemba 2019 na unatekelezwa katika mamlaka za serikali za mitaa 159 bara na visiwani.

Alisema idadi za kaya zilizopatiwa ruzuku zilikuwa milioni 1.1 zenye watu 5,296,470, ongezeko ikiwa uandikishwaji watoto 1,805,613 shule za msingi na sekondari ni 448,409.

Kuhusu mkataba wa pili, alisema lengo la programu ya mfuko wa pamoja wa afya ni kuimarisha mfumo wa huduma za afya ya msingi kwa kuwezesha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya na malengo yake.

Alisema pia inalenga kuboresha utendaji wa watoa huduma ya afya ya msingi, kuhakikisha huduma bora ya afya inatolewa.

"Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora ya afya na msingi na uwajibikaji kijamii, huu mfuko ulianzishwa mwaka 1999, mchango wa serikali ya Uswisi kwa miaka 10 iliyopita ni Dola za Marekani milioni 36.12, umeleta mafanikio makubwa kwa Watanzania maskini kwenye halmashauri 184," alisema.

Naye Balozi wa Uswisi nchini, Didier Chassot, alisema nchi yake na Tanzania zimekuwa na uhusiano mzuri wa kidiplomasia kwa muda mrefu tangu mwaka 1966.

"Wakati tunaipongeza Tanzania kwa kupiga hatua kiuchumi na kusababisha ubora wa hali ya maisha ya watu wengi, ni lazima tulinde maisha ya wale ambao hawajafaidika na ukuaji huu, hivyo Serikali ya Uswisi inaunga mkono agenda ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu ya kutomwacha yeyote nyuma."

Alisema ana imani kwamba kwa pamoja wataweza kufanikiwa zaidi na kuendelea kukuza na kuimarisha uhusiano kati ya nchi hizo.

Enabel

**Enabel – SAKIRP - Vacancy**

**Construction site supervisor - Kigoma region**

Enabel – the Belgian Development Agency is recruiting civil building technicians for the supervision of bridge construction works.

**Duty station:** Kigoma region Kakonko or Kibondo – willing to relocate in function of construction sites.
**Contract term:** 1 year extendable - competitive salary package(14 months' Salary i.e. Leave allowance and Christmas Bonus) Medical Insurance Coverage, Relocation allowance Etc.

**Profile:** minimum diploma in Civil Engineering or equivalent

**Experience:** minimum 2 years hands-on supervision of masons and contractors.
Computer literate and good reporting skills in English/ Kiswahili.
Details vacancy at: **https://btctanzania.wordpress.com/**
Submit your applications to: **recruitment.tza@enabel.be**

**Deadline: 20TH October 2020 at 15:00 HOURS**

**Only shortlisted candidates will be contacted.**

**TANGAZO**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## *KUMB: PPR/2020 – 10/1*

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 7 OKTOBA 2020

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia Jumatano, **Tarehe 7 Oktoba 2020**. Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za jumla na rejareja za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa kupitia **Bandari ya Dar es Salaam** zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 2 Septemba 2020. Kwa mwezi Oktoba 2020, bei za rejareja za Petroli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa Shilingi 25/lita (sawa na asilimia 1.35) na Shilingi 3/lita (sawa na asilimia 0.18), mtawalia, wakati bei ya Dizeli imepungua kwa shilingi 15/lita (sawa na asilimia 0.83). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei ya jumla ya Petroli imeongezeka kwa shilingi 18.91/lita (sawa na asilimia 1.09), wakati bei za jumla za Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 20.75/lita (sawa na asilimia 1.24) na Shilingi 2.99/lita (sawa na asilimia 0.19), mtawalia.

(b) Kwa mwezi Oktoba 2020, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimebadilika ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 2 Septemba 2020. Kwa mwezi Oktoba, bei za rejareja za Petroli na Mafuta ya Taa zimeongezeka kwa shilingi 4/lita (sawa na asilimia 0.20) na shilingi 14/lita (sawa na asilimia 0.71), mtawalia wakati bei ya Dizeli imepungua kwa shilingi 15/lita (sawa na asilimia 0.85). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa shilingi 2.27/lita (sawa na asilimia 0.13) na shilingi 21.07/lita (sawa na asilimia 1.28), mtawalia, wakati bei ya Mafuta ya Taa imeongezeka kwa shilingi 8.02/lita (sawa na asilimia 0.43).

(c) Kwa mwezi Oktoba 2020, bei za rejareja na jumla kwa bidhaa za mafuta ya Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi, and Ruvuma)** zimebadilika ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 2 Septemba 2020. Kwa mwezi Oktoba, bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimeongezeka kwa shilingi 8/lita (sawa na asilimia 0.40) na Shilingi 4/lita (sawa na asilimia 0.24), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei ya jumla ya Petroli imeongezeka kwa shilingi 1.53 (sawa na ailimia 0.09) wakati bei ya Dizeli imepungua kwa shilingi 1.73/lita (sawa na asilimia 0.10), mtawalia.

(d) Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia, gharama za usafirishaji (BPS Premium) na gharama za uendeshaji wa biashara ya mafuta.

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo *(price cap)*** kama ilivyokokotolewa na kanuni (formula) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 656 la tarehe 21 Agosti 2020.**

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP *(Electronic Fiscal Pump Printers)* na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

# TANGAZO

### JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| **Dar es Salaam** | **1,877** | **1,778** | **1,695** |
| **Arusha** | **1,909** | **1,815** | **2,058** |
| Arumeru (Usa River) | 1,909 | 1,815 | 2,058 |
| Karatu | 1,927 | 1,833 | 2,076 |
| Longido | 1,920 | 1,826 | 2,069 |
| Monduli | 1,914 | 1,820 | 2,063 |
| Monduli-Makuyuni | 1,919 | 1,825 | 2,068 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 1,994 | 1,900 | 2,143 |
| **Pwani (Kibaha)** | **1,882** | **1,783** | **1,700** |
| Bagamoyo | 1,888 | 1,789 | 1,706 |
| Bagamoyo (Miono) | 1,919 | 1,820 | 1,737 |
| Chalinze Junction | 1,891 | 1,792 | 1,709 |
| Chalinze (Msata) | 1,895 | 1,796 | 1,713 |
| Kibiti | 1,898 | 1,798 | 1,716 |
| Kisarawe | 1,884 | 1,785 | 1,702 |
| Mkuranga | 1,887 | 1,788 | 1,705 |
| Rufiji | 1,905 | 1,806 | 1,723 |
| **Dodoma** | **1,936** | **1,837** | **1,754** |
| Bahi | 1,943 | 1,844 | 1,761 |
| Chamwino | 1,931 | 1,832 | 1,749 |
| Chemba | 1,962 | 1,863 | 1,780 |
| Kondoa | 1,969 | 1,870 | 1,787 |
| Kongwa | 1,933 | 1,834 | 1,751 |
| Mpwapwa | 1,937 | 1,838 | 1,755 |
| Mtera (Makatopora) | 1,955 | 1,856 | 1,773 |
| Mvumi | 1,942 | 1,843 | 1,760 |
| **Geita** | **2,043** | **1,943** | **1,861** |
| Bukombe | 2,032 | 1,932 | 1,850 |
| Chato | 2,064 | 1,965 | 1,882 |
| Mbogwe | 2,081 | 1,982 | 1,899 |
| Nyang'hwale | 2,058 | 1,959 | 1,876 |
| **Iringa** | **1,941** | **1,842** | **1,759** |
| Ismani | 1,946 | 1,847 | 1,764 |
| Kilolo | 1,946 | 1,847 | 1,764 |
| Mufindi (Mafinga) | 1,951 | 1,852 | 1,769 |
| Mufindi (Igowole) | 1,960 | 1,861 | 1,778 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,093** | **1,994** | **1,911** |
| Biharamulo | 2,067 | 1,968 | 1,885 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,109 | 2,010 | 1,927 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,115 | 2,016 | 1,933 |
| Muleba | 2,093 | 1,994 | 1,911 |
| Ngara | 2,081 | 1,981 | 1,899 |
| Misenyi | 2,101 | 2,002 | 1,919 |
| **Katavi (Mpanda)** | **2,085** | **1,986** | **1,903** |
| Mlele (Inyonga) | 2,104 | 2,005 | 1,922 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,078 | 1,979 | 1,896 |
| Tanganyika (Ikola) | 2,103 | 2,004 | 1,921 |
| **Kigoma** | **2,109** | **2,010** | **1,927** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,121 | 2,022 | 1,939 |
| Buhigwe | 2,098 | 1,999 | 1,916 |
| Kakonko | 2,066 | 1,967 | 1,884 |
| Kasulu | 2,095 | 1,996 | 1,913 |
| Kibondo | 2,073 | 1,974 | 1,891 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **1,899** | **1,805** | **2,048** |
| Hai (Bomang'ombe) | 1,902 | 1,808 | 2,051 |
| Mwanga | 1,892 | 1,798 | 2,041 |
| Rombo (Mkuu) | 1,915 | 1,821 | 2,064 |
| Same | 1,885 | 1,791 | 2,034 |
| Siha (Sanya Juu) | 1,905 | 1,811 | 2,054 |
| **Lindi** | **1,908** | **1,834** | **1,754** |
| Lindi-Mtama | 1,912 | 1,838 | 1,772 |
| Kilwa Masoko | 1,932 | 1,857 | 1,729 |
| Liwale | 1,943 | 1,869 | 1,775 |
| Nachingwea | 1,928 | 1,853 | 1,783 |
| Ruangwa | 1,934 | 1,860 | 1,785 |
| **Manyara (Babati)** | **1,943** | **1,849** | **2,092** |
| Hanang (Katesh) | 1,954 | 1,860 | 2,103 |
| Kiteto (Kibaya) | 1,958 | 1,864 | 2,107 |
| Mbulu | 1,956 | 1,862 | 2,105 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 1,975 | 1,881 | 2,124 |
| **Mara (Musoma)** | **2,056** | **1,957** | **1,874** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,097 | 1,997 | 1,915 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,065 | 1,966 | 1,883 |
| Rorya (Shirati) | 2,099 | 2,000 | 1,917 |
| Bunda | 2,047 | 1,948 | 1,865 |
| Bunda (Kisorya) | 2,057 | 1,957 | 1,875 |
| Butiama | 2,053 | 1,954 | 1,871 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,101 | 2,002 | 1,919 |
| Tarime | 2,067 | 1,968 | 1,885 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,071 | 1,972 | 1,889 |
| **Mbeya** | **1,984** | **1,885** | **1,802** |
| Chunya | 1,994 | 1,895 | 1,812 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,008 | 1,909 | 1,826 |
| Kyela | 2,000 | 1,901 | 1,818 |
| Mbarali (Rujewa) | 1,968 | 1,869 | 1,786 |
| Rungwe (Tukuyu) | 1,993 | 1,894 | 1,811 |
| **Morogoro** | **1,902** | **1,803** | **1,720** |
| Mikumi | 1,918 | 1,819 | 1,736 |
| Kilombero (Ifakara) | 1,940 | 1,841 | 1,758 |
| Kilombero (Mlimba) | 1,962 | 1,863 | 1,780 |
| Kilombero (Mngeta) | 1,952 | 1,852 | 1,770 |
| Ulanga (Mahenge) | 1,951 | 1,852 | 1,769 |
| Malinyi | 1,961 | 1,862 | 1,779 |
| Kilosa | 1,921 | 1,821 | 1,739 |
| Gairo | 1,921 | 1,821 | 1,739 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 1,913 | 1,814 | 1,731 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 1,902 | 1,803 | 1,720 |
| Turiani | 1,927 | 1,828 | 1,745 |
| **Mtwara** | **1,894** | **1,820** | **1,768** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 1,931 | 1,856 | 1,816 |
| Masasi | 1,910 | 1,836 | 1,793 |
| Newala | 1,915 | 1,841 | 1,800 |
| Tandahimba | 1,908 | 1,834 | 1,793 |
| Nanyamba | 1,908 | 1,834 | 1,793 |
| **Mwanza** | **2,027** | **1,928** | **1,845** |
| Kwimba | 2,045 | 1,946 | 1,863 |
| Magu | 2,035 | 1,936 | 1,853 |
| Misungwi | 2,022 | 1,923 | 1,840 |
| Sengerema | 2,060 | 1,961 | 1,878 |
| Ukerewe | 2,087 | 1,988 | 1,905 |
| **Njombe** | **1,970** | **1,871** | **1,788** |
| Njombe (Kidegembye) | 1,990 | 1,891 | 1,808 |
| Ludewa | 2,008 | 1,908 | 1,826 |
| Makambako | 1,962 | 1,863 | 1,780 |
| Makete | 2,000 | 1,901 | 1,818 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 1,967 | 1,868 | 1,785 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,050** | **1,951** | **1,868** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,050 | 1,951 | 1,868 |
| Kalambo (Matai) | 2,057 | 1,958 | 1,875 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,064 | 1,965 | 1,882 |
| **Ruvuma (Songea)** | **1,980** | **1,906** | **1,819** |
| Mbinga | 1,992 | 1,918 | 1,852 |
| Namtumbo | 1,971 | 1,897 | 1,848 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,018 | 1,944 | 1,862 |
| Tunduru | 1,945 | 1,871 | 1,878 |
| **Shinyanga** | **2,006** | **1,907** | **1,824** |
| Kahama | 2,020 | 1,921 | 1,838 |
| Kishapu | 2,035 | 1,935 | 1,853 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,037 | 1,938 | 1,855 |
| Salawe | 2,021 | 1,922 | 1,839 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **2,048** | **1,949** | **1,866** |
| Busega (Nyashimo) | 2,041 | 1,941 | 1,859 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,051 | 1,952 | 1,869 |
| Maswa | 2,039 | 1,940 | 1,857 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,046 | 1,947 | 1,864 |
| **Singida** | **1,968** | **1,869** | **1,786** |
| Iramba | 1,980 | 1,881 | 1,798 |
| Manyoni | 1,953 | 1,853 | 1,771 |
| Itigi (Mitundu) | 1,968 | 1,869 | 1,786 |
| Ikungi | 1,963 | 1,864 | 1,781 |
| Mkalama (Nduguti) | 1,992 | 1,893 | 1,810 |
| **Songwe (Vwawa)** | **1,994** | **1,894** | **1,812** |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,000 | 1,901 | 1,818 |
| Ileje | 1,997 | 1,898 | 1,815 |
| Momba (Chitete) | 2,003 | 1,904 | 1,821 |
| Tunduma | 1,998 | 1,899 | 1,816 |
| **Tabora** | **2,031** | **1,932** | **1,849** |
| Igunga | 1,985 | 1,886 | 1,803 |
| Kaliua | 2,050 | 1,951 | 1,868 |
| Ulyankulu | 2,045 | 1,945 | 1,863 |
| Nzega | 1,996 | 1,897 | 1,814 |
| Sikonge | 2,043 | 1,944 | 1,861 |
| Urambo | 2,045 | 1,945 | 1,863 |
| Uyui | 2,032 | 1,933 | 1,850 |
| **Tanga** | **1,852** | **1,758** | **2,001** |
| Handeni | 1,873 | 1,779 | 2,022 |
| Kilindi | 1,888 | 1,794 | 2,037 |
| Korogwe | 1,865 | 1,770 | 2,013 |
| Lushoto | 1,874 | 1,780 | 2,023 |
| Mkinga (Maramba) | 1,859 | 1,765 | 2,008 |
| Muheza | 1,857 | 1,763 | 2,006 |
| Pangani | 1,859 | 1,765 | 2,008 |

### JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | 1,746.19 | 1,647.01 | 1,564.98 |
| TANGA | 1,721.57 | 1,627.36 | 1,870.21 |
| MTWARA | 1,763.29 | 1,688.87 | -- |

**Mha. Godfrey H. Chibulunje**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sekta mifugo ichochee safari uchumi mkubwa

**WAKATI** Tanzania inaelekeza jitihada zake kufikia uchumi mkubwa kwa lugha nyingine, uchumi wa viwanda, mipango na mikakati sasa hainabudi kuiangalia sekta ya mifugo kwa jicho la pili.

Hiyo ni kutokana na sekta ya mifugo kuwa na fursa nyingi za kuwezesha viwanda vyetu kuzalisha zaidi, kupitia kuvipatia malighafi zinazotokana na mazao yanayopatikana ikiwamo nyama, maziwa na ngozi.

Kwa sasa Tanzania inatajwa kuwa nchi ya pili kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo barani Afrika. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Prof. Hezron Nongwa, kwa wahariri wa vyombo vya habari, Tanzania ina zaidi ya ng'ombe milioni 33, mbuzi milioni 22, kondoo milioni 5.6, punda zaidi ya 600,000, kuku milioni 83 na nguruwe 2,000,000.

Alieleza pia kwamba sekta ya mifugo kwa sasa inachangia asilimia 7.5 katika pato la taifa. Takwimu hizo na mchango wa sekta hiyo kwa pato la taifa ni ujumbe tosha kuhusiana na umuhimu wake katika safari ya kuelekea kwenye uchumi mkubwa wa viwanda baada ya nchi yetu kufanikiwa kuingia rasmi katika uchumi wa kati hivi karibuni.

Hatua kadhaa tunaona kuwa lazima zichukuliwe na serikali, wataalamu, wafugaji na wadau wengine kuboresha na kuipaisha sekta ya ufugaji ili iweze kuchangia inavyostahili katika safari ya uchumi wa viwanda. Kwa kiasi fulani kuna mafanikio yamepatikana kwa upande wa chanzo cha magonjwa mbalimbali ya mifugo, ingawa lengo la serikali ni kupata chanjo za magonjwa yote 13 ya mifugo. Magonjwa ya mifugo yanatajwa kuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya mifugo, ambapo Prof. Nongwa anasema magonjwa yanachangia vifo vya mifugo kwa asilimia 60.

Katika jitihada hizo, Taasisi ya Chanjo ya Kibaha mkoani Pwani, imeanza kuzalisha matokeo chanya baada ya kuonekana kufanikiwa kudhibiti kwa asilimia 95 ugonjwa wa mdondo unaowapata kuku wa kufuga.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari waliotembelea katika taasisi hiyo kushuhudia shughuli za utengenezaji wa chanjo za kudhibiti magonjwa ya mifugo zinazofanywa na taasisi hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Sekta ya Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema mafanikio hayo ni kwa wafugaji waliozingatia kuchanja kuku wao mara tatu kwa mwaka kama inavyoelekezwa na wataalam wa mifugo.

Pia inaelezwa kuwa chanjo hiyo pia imesaidia kudhibiti ugonjwa wa ndorobo kutoka asilimia 32 hadi asilimia 60 katika maeneo mbalimbali nchini, yakiwamo ya hifadhi za taifa, kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania, Dk. Furaha Mramba. Tunaipongeza serikali kwa kuamua kuweka msukumo kwa kuamua kuzalisha chanjo nchini kwa kuwa hatua hiyo itaepusha uwezekano wa hujuma za kiusalama ikiwa zitatoka nje pamoja na gharama kubwa za kuziagiza nje.


Ushauri wetu ni kuwa serikali iendelee kuiwezesha Mamlaka ya Maabara ya Veritenari Tanzania kibajeti ili itekeleze mkakati maalum wa kuzalisha chanjo za magonjwa yote 13.

Hatua nyingine muhimu ya kuhimiza na kuzingatiwa ni kwa wafugaji kujenga utamaduni wa kuwashirikisha na kuwatumia wataalamu wa mifugo kujua chanzo sahihi cha magonjwa yanayoikabili mifugo yao badala ya kujigeuza wao madaktari wa mifugo.

Hilo ni miongoni mwa mambo ambayo Prof. Gabriel, aliyahimiza, kwa kusema kuwa kuna baadhi ya wafugaji wanadhani kuwa ng'ombe ni wao, wanadhani wanaweza kuwa madaktari wakati sio kweli. Kwamba wafugaji lazima wawatumie wataalamu wa mifugo waambiwe chanzo sahihi kinachoikabili mifugo yao badala ya kukimbilia kuwapa chanjo au dawa wanazozijua wenyewe wakati sio za kweli.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Uchaguzi usiwe sababu kuua, kushambuliana

Na Sabato Kasika

**TANZANIA** inasifika kote duniani kwa kuwa kisiwa cha amani, kutokana na umoja na mshikamano wa wananchi wake, wanaojiona na kujitambulisha zaidi kama Watanzania kuliko dini au makabila ya asili.

Amani, utulivu na mshikamano wa Watanzania, vimekuwa ni wimbo wa kila siku wa viongozi wa serikali, dini na wengine kwa lengo la kuendelea kuvienzi kwa manufaa ya vizazi vilivyo na vijavyo.

Hata hivyo, wakati huu wa kampeni za uchaguzi mkuu zinazoendelea inadiwa kuwapo kwa baadhi ya vitendo ambavyo visipodhibitiwa vinaweza kuhatarisha amani, utulivu na mshikamano huo.

Juzi wakati anatoa tathmini ya mwenendo wa kampeni za uchaguzi Bara na visiwani Zanzibar, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, anaelezea kusikitishwa na vitendo hivyo.

Anasema, CCM imetishwa na mauaji kwa vijana wake yaliyoripotiwa kwenye mikoa mwili Bara na tukio la kushambuliwa viongozi wake kwa mapanga kisiwani Pemba wakati wakiwa kwenye ibada msikitini.

"Licha ya hujuma wanazofanyiwa wana CCM kwa kupigwa na kuuliwa, lakini chama hakitolipiza kisasi na kinaendelea kuhubiri amani na utulivu," ndivyo anavyosema Dk. Bashiru.

Kama matukio hayo yapo, ni muhimu kwa wasaka madaraka wote hao kujiepusha nayo katika hatakati za kutaka kuungwa mkono, badala yake waeneze sera na ilani za vyama vyao tu.

Tanzania ni kisiwa cha amani, Watanzania wote wajivunie kuwa katika nchi ya amani duniani badala ya kuingiza mambo yanayoweza kusababisha itoweke, kwa sababu tu ya watu fulani wanataka madaraka.

Hivyo kuelekea uchaguzi mkuu, wote hawana budi kuhimiza amani, na uwe ni wimbo wa kila mmoja, ili hatimaye kampeni na uchaguzi mkuu vifanyike na kumalizika kwa amani.

Ni vyema kukumbushana kwamba, utulivu, amani na mshikamano ni muhimu katika kuwezesha maendeleo endelevu, kama ambavyo vurugu ama ghasia ni moja ya vikwazo katika maendeleo.

Kwa hiyo vijana ambao kimsingi ndiyo wenye nguvu, wasikubali kutumika kama madaraja ya wanasiasa kufanikisha malengo yao, hasa kwenye uchaguzi huu wasitumike kwa manufaa ya wanasiasa, bali kwa manufaa ya taifa.

Zaidi ya hapo vijana wahamasishwe kuendeleza amani kwa kusikiliza pia maelekezo ya viongozi wa dini ambayo yamejikita zaidi kwenye amani na utulivu wa nchi hii ambao umedumu kwa miaka mingi.

Vijana ni chachu ya mabadiliko, lakini mabadiliko yafanywe kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria na siyo kulazimisha, bali viongozi wao wawaelekeze kutumia nguvu ya hoja, siyo kutumika kufanya vurugu.

Kinachotakiwa ni wao kujitambua na kujiamini ili wakatae kutumika kuhatarisha amani ya nchi na kusababisha Watanzania kuishi kwa hofu, kwa sababu ya kuwanufaisha watu fulani.

Watambue kuwa wapo baadhi ya wanasiasa, walioko tayari kutumia njia zozote zile zikiwamo chafu kwa ajili ya kupata madaraka, hivyo wawe tayari kuwaepuka wasiwaingize mtegoni.

Hivyo wakati huu wa kuelekea kufikia siku ya uchaguzi mkuu wakati wanasiasa wanaendelea na harakati za kusaka nafasi za urais, ubunge na udiwani, suala la amani, utulivu na mshikamano ni muhimu kuhimizwa.

Kwa hali hiyo wanasiasa watumie siku za kampeni zilizosalia kuhakikisha vijana wanajitenga na mambo ambayo yanaweza kuhatarisha amani na kuiingiza nchi kwenye hatari ya kusambaratisha umoja wa Watanzania.

Vijana ambao kimsingi ni nguvukazi ya taifa na ambao hutumiwa na wanasiasa wanatakiwa kujitenga na kuwapuuza ili wasisababishe mgawanyiko miongoni mwa Watanzania, kwa maslahi ya watu binafsi.

Tusisubiri kujenga ukuta, bali tuzibe nyufa ambazo zimeanza kujitokeza zenye lengo la kuwagawa Watanzania ili wasiwe wamoja na pia waogopwe wagombea wanaotafuta nafasi kwa kuwagawa Watanzania.

Kumbuke Tanzania yenye amani, utulivu na mshikamano inawezekana, kinachotakiwa ni wasiasa kuwa na akiba na maneno katika kampeni zao ili yasiwe simu kwa ustawi wa nchi hii.

HABARI KITAIFA

## ‘Watoto kusimamia harusi ni ukatili kijinsia’

**Na Christina Mwakangale**

JAMII imetakiwa kutambua kuwa kuhusisha watoto wadogo kwenye usimamizi wa sherehe za harusi wakati wa kufunga ndoa ni ukatili wa kijinsia.

Naibu Msajili Mahakama Kuu ya Tanzania, Kitengo cha Watoto, Hakimu Nyigulila Mwaseba, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam, wakati akiwasilisha mada kuhusu uendeshaji wa kesi za watoto.

Alisema imezoeleka kwenye jamii kuwatumia watoto katika shughuli hizo na kwamba kitendo hicho kinachangia kuporomoka kwa maadili ya watoto.

“Bibi harusi na bwana harusi wadogo, yaani watoto wanaosimamia ni ukatili wa kijinsia. Sherehe hizi hufanyika hadi usiku sana, inawakosesha haki yao ya kupumzika.”

“Wakati maharusi wanainuka kucheza nao wanaambiwa wacheze tena muziki wa ‘blues’, tunaanza kuwaharibu watoto kimaadili mapema,” alisema Mwaseba.

Kadhalika, alifafanua kuwa kitendo cha kumtuma mtoto kwenda dukani kununua vilevi ikiwamo pombe na sigara ni kosa la jinai.

“Watoto ni kundi maalumu kati ya makundi maalumu yanayotambulika kwenye jamii na sheria zinawalinda, kanuni na kifungu namba 95 inasema ni wajibu wa kutoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa haki za mtoto,” alisema Mwaseba.

Hakimu Mkazi Mwandamizi kutoka Mahakama Kuu, Rhoda Ngamilanga, akizungumza kwenye semina ya ngazi ya jamii (GDSS) zinazoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), alisema ukatili wa kijinsia unamwathiri kisaikolojia anayetendewa.

# Milioni moja kufanya mtihani darasa la VII

**Romana Mallya na Frank Maxmillian**

WATAHINIWA 1,024,007 wanatarajia kuanza Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) leo, wasichana wakiwa 530,718, sawa na asilimia 51.83.

Kwa mwaka jana, idadi ya watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani huo ilikuwa 947,077.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Dk. Charles Msonde, katika mkutano wake na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema wavulana wanaotarajiwa kufanya mtihani huo wa siku mbili (leo na kesho) ni 493,289, sawa na asilimia 48.17.

Dk. Msonde alisema watahiniwa waliosajiliwa kufanya mtihani huo kwa lugha la Kiswahili ni 974,532 na kwa lugha ya Kiingereza ni 49,475.

“Watahiniwa wenye uhitaji maalum wapo 2,943. Kati yao, 86 ni wasioona, 895 wenye uoni hafifu, 739 wenye ulemavu wa kusikia, 286 ni wenye ulemavu wa akili na 937 wenye ulemavu wa viungo vya mwilini,” alisema.

Kiongozi huyo alisema katika mtihani huo, masomo matano yatatahiniwa, ambayo ni Kiswahili, Kiingereza, Sayansi, Hisabati na Maarifa ya Jamii.

“Mtihani huo utafanyika katika shule 17,335 za Tanzania Bara. Maandalizi yote yamekamilika ikiwa ni pamoja na kusambazwa kwa karatasi za mitihani, fomu maalum za kujibia mtihani na nyaraka zote muhimu, zinazohusu mtihani huo katika halmashauri,” alisema.

Dk. Msonde alitoa wito kwa kamati za mitihani za mikoa na halmashauri, manispaa na jiji kuhakikisha kuwa taratibu zote za uendeshaji zinazingatiwa ipasavyo.

“Kamati zihakikishe mazingira ya vituo vya mitihani yako salama, tulivu na kuzuia mianya yote inayoweza kusabaisha kutokea kwa udanganyifu, hakikisheni usalama wa vituo unaimarishwa, vitumike kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na baraza,” aliagiza.

Dk. Msonde pia, alitoa wito kwa wasimamizi walioteuliwa, kufanya kazi zao kwa umakini na uadilifu kwa kuzingatia kanuni za mitihani na miongozo waliyopewa.

“Mhakikishe mnalinda haki za watahiniwa wenye uhitaji maalum, haki hizo ni pamoja na kuwapa mitihani yenye maandishi ya nukta nundu kwa watahiniwa wasioona na maandishi yaliyokuzwa kwa wenye uoni hafifu,” alisema.

Aliagiza kwa watahiniwa wote wenye uhitaji maalum, waongezwe muda wa dakika 20 kwa kila saa kwa somo la Hisabati na dakika 10 kwa kila saa kwa masomo mengine.

Dk. Msonde alisema baraza linawataka wamiliki wa shule kutambua kuwa, shule zao ni vituo maalum vya mitihani na hawatakiwi kwa namna yoyote kuingilia majukumu ya wasimamizi wa mitihani.

Alisema baraza halitasita kukifuta kituo chochote cha mitihani endapo litajiridhisha pasipo shaka kuwa uwapo wake unahatarisha usalama wa mitihani ya taifa.

Pia, alisema hawatasita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayebainika kujihusisha au kusababisha udanganyifu wa mitihani.

“Tunawaomba wadau watoe taarifa katika vyombo husika kila wanapobaini uwapo wa mtu au kikundi cha watu kujihusisha na udanganyifu wa mitihani,” alisema.



# W/biashara mazao ya misitu sasa wahakikishiwa soko

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), imewahakikishia wafanyabiashara wa mazao yatokanayo na misitu, mazingira bora ya soko ndani na nje ya nchi.

Naibu Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Mohamed Kilongo, alisema Wakala huo utahakikisha kwamba wafanyabiashara hao wanapata bidhaa bora kwa ajili ya kutengeneza samani zenye kiwango cha juu kwa ajili ya kuuza nje ya nchi.

Alisema yapo mazao ya misitu mengi na bora katika mashamba ya serikali na kwamba lengo lao ni kuhakikisha wanawawezesha wafanyabiashara hao kuyatumia kutengeneza samani zenye viwango vya kimataifa.

"Maelekezo ya sasa ya serikali ni kuhakikisha samani zinazotumika ni zile zinazotokana na mazao ya misitu yetu ya ndani na zilizotengenezwa hapa kwetu, kwa hiyo kazi iliyopo kwa sasa ni kwa wafanyabiashara wenyewe kuchangamkia fursa hii," alisema Kilongo.

"Serikali kupitia TFS, imejipanga kuhakikisha wafanyabiashara katika sekta hii wanapata mazao ya misitu yenye ubora ambao unahitajika ndani ya nchi yetu, lakini na kimataifa."

Alisema TFS imeandaa utaratibu mzuri ambao utawasaidia wafanyabiashara wote katika sekta hiyo ya misitu ikiwamo wanaotengeneza samani, kununua miti yenye ubora kutoka katika mashamba ya serikali.

Alisema utaratibu huo amabo umewekwa kwa sasa ni pamoja na kufanya mialiko maalum ya mara kwa mara kwa wafanyabiashara hao kwa ajili ya uuzaji wa miti hiyo kwa uwazi.

Alisema lengo ni kurahisisha kila mfanyabiashara apate fursa ya kununua miti anayoihitaji kulingana na aina ya samani anazotengeneza na pia kusaidia kuepusha mianya ya kuwapo urasimu wakati wa uuzaji wa mazao ya misitu.

Mhifadhi wa Wakala huo kutoka Shamba la Miti la Mtibwa, Abdala Mchomvu, alisema lengo lao wanataka kuwaondoa wafanyabiashara wa mazao hiyo katika fikra ya mazoea ya kuamini katika bidhaa za miti za aina moja.

"Tanzania tuna aina nyingi za mazao ya miti ambayo ni bora sana, lakini cha kushangaza ni kwamba wafanyabiashara wetu wamezoea aina fulani tu ya miti kwamba ndiyo bora, tutaendelea kuwaelimisha na tunaamini watabadilika kwa sababu yapo mazao ya miti ya aina nyingi na ni bora," alisema Mchomvu.

## Tigo yajivunia ufanisi huduma wiki ya wateja

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano inayoongoza kwa kutoa huduma za kidigitali nchini, Tigo Tanzania, inaadhimisha wiki ya huduma kwa wateja kwa kutambua na kusherehekea huduma nzuri zinazotolewa na wafanyakazi wake.

Wafanyazi hao wa kitengo cha huduma kwa wateja siku zote wapo mstari wa mbele kuipeperusha bendera ya kampuni hiyo, kwa wateja kupitia njia mbalimbali za mawasiliano.

Sherehe hizi za wiki zima zitaenda sambamba na kauli mbiu ya mwaka huu ambayo ni 'Dream Team'.

Akizungumza katika kituo cha kuzungumza na watoa huduma wa Tigo, Mkuu wa Kitengo cha huduma kwa wateja wa Tigo Tanzania, Mwangaza Matotola, alisema maadhimisho ya mwaka huu yatafanyika kwa kuonyesha ubora wa watoa huduma wa kampuni hiyo kwa wateja.

"Mwaka huu umekuwa mwaka uliojaa changamoto nyingi kwa wafanyakazi wetu wa kitengo cha huduma kwa wateja, wamejitahidi kuwa pamoja kuhakikisha maswali kutoka kwa wateja wetu yanapatiwa majibu haraka," alisema.

Aliongeza kusema kwamba, pia waliwaomba wateja wao kuendana na mazingira yaliyokuwepo kwa kujikita zaidi katika matumizi ya huduma za kimtandao.

"Hivyo pongezi nyingi ziende kwa timu yetu ya huduma kwa wateja kwa kutoa huduma kwa wateja wetu zenye ubora mkubwa," alisema Matotola.

Wiki ya huduma kwa wateja ya Tigo Tanzania itaambata na shughuli mbalimbali ikiwemo kuchati moja kwa moja na wateja na pia kukuna na wataja pamoja na wadau wengine.

Alisema kila wanapopata changamoto yoyote ya kimawasiliano, wateja wa Tigo wanashauriwa kutembelea maduka ya kampuni yaliyoko nchi nzima, lakini pia kupata huduma kupitia njia nyingine za mawasiliano kama vile kuongea na mtoa huduma au kuchati kupitia WhatsApp, Instagram, Twitter na Facebook.



Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania PLC, Hisham Hendi (wa pili kushoto), akikabidhi tuzo za kutambua mchango wa tasnia ya habari kwa mwakilishi wa kampuni ya The Guardian Ltd inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Frank Monyo, wakati wa hafla ya maadhimisho ya miaka 20 ya Vodacom Tanzania, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa kampuni hiyo, Rosalynn Mworia (kushoto) na Mkurugenzi wa Biashara wa Vodacom, Linda Riwa. **MPIGAPICHA WETU**

# Vodacom yatoa tuzo kusherehekea miaka 20

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Vodacom imetoa tuzo kwa Kampuni ya The Guardian Limited kwa kutambua mchango wake wa kuhabarisha umma juu ya huduma wanazotoa kwa jamii tangu kuanzishwa kwake.

Tuzo hiyo imekabidhiwa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Vodacom, Hisham Hendi, wakati wa sherehe ya maadhimisho ya kutimiza miaka 20 ya utoaji huduma bora Tanzania.

Alisema Vodacom inatambua mchango mkubwa uliotolewa na vyombo vya habari hasa Kampuni ya The Guardian LTD katika kuhakikisha umma unafahamu huduma bora zinazotolewa na kampuni hiyo, kwa kipindi cha miaka 20.

"Zaidi ya miaka 20 sasa Vodacom imekuwa ikishiriki na kuwa mstari wa mbele katika kuwaunganisha Watanzania hapa nyumbani na hata nje ya nchi na vyombo vya habari vimekuwa msaada mkubwa kwetu. Kama kaulimbiu yetu ya yajayo yanafurahisha na kama Brand tunasema lengo letu ni kuwaunganisha Watanzania kupitia teknolojia kwa maisha bora yajayo, alisema Hendi.

Vodacom imetoa tuzo 22 kwa vyombo vya habari ambazo zimefanya kazi kwa pamoja katika muda wa miaka 20 sasa. Kati ya kampuni zilizopokea tuzo ni The Guardian Limited, Eatv, ITV na vyombo vingine vya habari.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Idara ya Biashara Vodacom, Linda Riwa, alisema katika kusherehekea miaka 20 ya kampuni hiyo wamezindua kampeni inayokwenda kwa jina la PAMOJA TUYAJENGE YAJAYO yenye lengo la kuboresha maisha ya Watanzania kwenye nyaja ya teknolojia na kutoa huduma bora.

"Pamoja Tuyajenge Yajayo ni kampeni inayolenga kuonyesha ni namna gani teknolojia inachangia mabadiliko katika nyanja mbalimbali. Na sisi kama Vodacom tunaamini na tumejipanga kuhakikisha tunasonga na Watanzania kwa pamoja kutumia mabadiliko haya chanya kabisa," alisema Riwa.

Alisema Vodacom inasherehekea na kuzindua kampeni hiyo kwa kukuza sekta ya teknolojia na mawasiliano kwa mtazamo wa kuangalia mbele zaidi. "Sisi na Watanzania kwa pamoja tutajenga yajayo ili kuijenga Tanzania ya Kidigitali na ndio maana tunasema Pamoja Tuyajenge Yajayo," alisema.

Akielezea safari ya miaka 20 tangu kuanza kutoa huduma kwa jamii, Mkurugenzi Mkuu wa Masuala ya Ushirika wa Vodacom, Rosalynn Mworia, alisema mtandao wa Vodacom umesambaa nchi nzima kwa kasi ya 4G na upatikanaji wa simu janja za bei nafuu. Watanzania wanafanya mengi kupitia mtandao huo.

Alisema Vodacom ni mtandao wa mawasiliano unaoongoza Tanzania ambao umekuwa ukiwahudumia wateja tangu Agosti 2000 na kumekuwa na maendeleo kuanzia kwenye mtandao wenye kasi ya 2G mpaka 4G+, simu za kawaida mpaka simu janja zenye sifa za kipekee.

Alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa kampuni hiyo wameweka kutoa ajira 2037 na wafanyakazi huru wanaolipwa kila mwezi wakiwa ni 28,500 huku mawakala mpaka kufikia Septemba mwaka huu walikuwa 130,000.



## RC aitaka NCBA kuchochea biashara

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ameitaka Benki ya NCBA kusaidia maendeleo ya sekta ya biashara kwa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa.

Mongella alitoa wito huo mwishoni mwa wiki wakati akizindua matawi mawili mapya ya benki hiyo, mkoani humo yaliyopo katika Barabara ya Nyerere na Jengo la Kauma, Barabara ya Kenyatta.

"Ni imani yetu kuwa Benki ya NCBA kama taasisi ya fedha itakuwa moja ya washirika bora, watakaowezesha wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa kusonga mbele katika hatua mpya ya maendeleo na kukuza pato la Taifa," alisema Mongella.

Kadhalika aliipongeza benki ya NCBA kwa ujio wao wa kihistoria kwenye mkoa huo na Taifa kwa ujumla.

"Ujio wenu kama benki mpya utasaidia kuanzisha na kukuza miradi mipya pamoja na kutoa programu mpya za kifedha zitakazokuza uwezo wa kiuchumi wa watu wa Mwanza na kuleta thamani zaidi katika vipaumbele

vya uchumi na shughuli za uzalishaji," alisema Mongella.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya NCBA, Margaret Karume, aliwahakikishia wadau, wageni na wateja kuwa benki inatoa huduma bora za kiwango cha kimataifa mahali popote walipo.

Kadhalika alimshukuru mkuu wa mkoa huo kwa utayari wao wa kuiunga mkono benki ya NCBA katika kuleta mageuzi ya kiuchumi ya mkoa huo.

## Shule kufundisha stadi za kazi, ujuzi

**Na Yasmine Ptotace,** MKURANGA

MWONGOZO wa miaka 10, umeandaliwa kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari St. Mathew's ambapo wanafundishwa stadi za kazi pamoja na ujuzi.

Mbali na kuwafundisha stadi za kazi na ujuzi, pia wameanza kufundishwa somo la Kichina.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa shule hiyo, Peter Mutembei, katika mahafali ya 20 ya kidato cha nne katika shule hiyo.

"Tumeshaandaa mwongozo wa miaka 10, ambao utaenda mpaka miaka 30, lengo ni kuongeza ubora katika elimu...wanafunzi watajifunza ujuzi na stadi za kazi," alisema.

Aliongeza kuwa, wanafunzi watakapokuwa wamepata ujuzi hali hiyo itawasaidia kutokaa vijiweni.

Aliongeza kuwa pia somo la Kichina linalotolewa katika shule yao, ambapo kwa sasa wanafunzi 17 wapo China kupitia ufadhili wa shule kupatiwa mafunzo.

Alisema baada ya kugundua kuwa wahitimu wanapomaliza masomo yao wanakaa vijiweni na wengine kujiingiza katika makundi yasiyofaa.

"Ili watoto wasiteketee vijiweni, tunaona ni bora kuanzisha masomo ya stadi za kazi na ujunzi lengo ni kuwa mkombozi huko waendapo. Wameshajifunza kutengeneza sabuni, mafuta, CCTV camera na kupiga picha," alisema.

Aliongeza kuwa, mpango huo, waliouanzisha utawasaidia watoto kujiongezea kipato na kutoshinda vijiweni.

# TOSCI yaonya uuzaji wa mbegu holela

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

TAASISI ya kudhibiti ubora wa mbegu Tanzania (TOSCI) imewaonya wauzaji holela wa mbegu za kilimo kwenye maeneo ambayo hayajaidhinishwa na serikali na uvunjaji wa taratibu za uhifadhi unaosababisha athari za kiafya kwa binadamu na hasara kwa wakulima.

**TOSCI wametusaidia sana kwa hiyo unanunua mbegu ambazo una uhakika hauvunji taratibu zilizowekwa na serikali.**

Akiwa mkoani Kigoma kwenye ziara ya kikazi ya kukagua maduka yanayouza mbegu, Ofisa Mfawidhi kutoka TOSCI Kanda ya Ziwa na Magharibi, Joseph Ngula, alisema kumekuwapo na baadhi ya watu wanaochanganya mbegu hizo na bidhaa nyingine za majumbani wakati wa kuuza jambo ambalo ni hatari kwa afya ya mlaji.

"Mkulima asinunue mbegu kwenye duka lolote lile kuna wengine wamethubutu kuchanganya na bidhaa zingine kama sukari na mchele ni hatari kwa mlaji," alisema Ngula.

Alisema licha ya kwamba mbegu hizo zimehifadhiwa vizuri, lakini katika harakati za kusafirisha vifungashio vinaweza kutoboka na endapo zitachanganywa na bidhaa zingine madhara ya kiafya yanaweza kutokea kutokana na mbegu hizo.

Ngula alieleza sababu nyingine ya kutokununua mbegu kiholela ni mkulima kuepukana na hasara kwani endapo atafuata taratibu husika na kudai risiti, tatizo likitokea kama mbegu kutokuota anaweza kufuatilia na kupata fidia kutoka kwa muuzaji.

Naye muuzaji wa mbegu kutoka Manispaa ya Kigoma/Ujiji, Wilson Richard, alisema TOSCI imekuwa ikiongeza ubora wa utoaji mafunzo kwao na kuwawezesha kuwa na elimu sahihi juu ya mbegu ambayo wamekuwa wakiitoa kwa wateja wao ambao ni wakulima.

Alisema wanafuata taratibu mbalimbali zinazoelekezwa ikiwamo kurudisha mbegu zikahakikiwe uwezo na ubora wa kuota kila baada ya miezi sita hadi saba kama wanavyoagiza.

"TOSCI wametusaidia sana kwa hiyo unanunua mbegu ambazo una uhakika hauvunji taratibu zilizowekwa na serikali," alisema.

Ukaguzi wa maduka yanayouza pembejeo umebaini kukua kwa uelewa wa wauzaji wa mbegu na ufuataji wa taratibu zilizowekwa japo baadhi ya wauzaji wamekutwa na mapungufu, ambayo wametakiwa kuyarekebisha ili kuendana na taratibu.



Madereva wa bajaj na bodaboda wakivuka alama za pundamilia kwa kukokota vyombo vyao, eneo la Manzese Bakhresa, jijini Dar es Salaam juzi, ikiwa ni sehemu ya utii wa sheria za usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Mgombea ACT ajinadi kumaliza kero Masasi

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Masasi Mjini kupitia ACT-Wazalendo, Musa Mwadewa, amesema endapo atapata ridhaa ya kuchaguliwa atashughulikia kero za ukosefu wa dawa kwenye vituo vya afya.

Kero nyingine amezitaja kuwa ni wajasiriamali kukosa mitaji na ukosefu wa majisafi na salama katika baadhi ya vijiji kwa kuwa zimekuwa ni matatizo sugu kwa wananchi.

Mwadewa aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na gazeti hili katika mahojiano maalumu kuhusu vipaumbele vyake atakavyovitekeleza iwapo akichaguliwa.

Aliipongeza serikali kwa kujenga vituo vingi vya afya na hospitali za wilaya na kanda nchini, lakini changamoto kubwa aliyoiona kwenye sekta ya afya katika jimbo hilo ni upatikanaji wa dawa kwenye vituo vya afya.

Mwadewa alisema akichaguliwa atashughulikia kero zote sugu ikiwamo upatikanaji wa dawa kwenye vituo vyote vya afya ambavyo wananchi wamekuwa wakienda kupata huduma za afya, lakini wamekuwa wakikosa dawa na kuelezwa kwenda kununua kwenye maduka binafsi.

Alisema kwa upande wa suala la uchumi amekuja na mikakati madhabuti ya kuinua uchumi kwa vijana na wanawake, ambapo atashughulikia changamoto za wajasiriamali wadogo ambao wanakosa fursa ya mitaji ya kuendeleza biashara zao, hivyo atawapatia elimu ya biashara pamoja na mikopo ili kukuza biashara zao.

Mwadewa alisema wajasiriamali wengi kwa sasa ndani ya jimbo hilo hasa wanawake wamekuwa wakitembea mitaani huku wakiwa wamebeba matenga na mabeseni ya biashara ndogo ambazo mitaji yao ni midogo, hivyo lazima wapatiwe mikopo ili kukuza biashara zao.

Alisema katika elimu atahakikisha watoto wote wa familia maskini ambao wamekuwa wakiacha shule kwa kukosa mahitaji ya msingi kama chakula, sare na daftari atasaidia watoto hao wanarejeshea shule na mahitaji hayo atagharamikia yeye kupitia fedha za mfuko wa jimbo.





# ‘Vipanya’ marufuku katikati Jiji Mwanza

**Na Richard Makore,** MWANZA

MAMLAKA ya Usimamizi wa Usafiri Ardhini (LATRA), imetangaza kuondoa magari yote madogo ya kusafirisha abiria ‘vipanya’ katikati ya jiji ifikapo mwakani, ili kuondoa msongamano na hivyo kuboresha sekta ya usafirishaji.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake, Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Mwanza, Ngereza Pateli, alisema mpango huo ulianza mwaka 2018.

Alisema tangu wakati huo, wamekuwa wakiratibu suala hilo na kwamba na wafanyabiashara kushindwa kujitokeza kununua magari makubwa yanayobeba abiria kuanzia 25.

Pateli alisema walipoanza mpango huo walikubaliana na wafanyabiashara hao kwamba wasitoe usijali kwa magari madogo mapya.

**Yapo mengi ambayo chama kimeahidi kupitia katika ilani, miongoni mwake ikiwa ni kuboresha maisha ya Watanzania, hasa wanyonge kwa kuwapa mikopo bila riba wala dhamana.**

Aliongeza kwamba mpango huo umelenga kufikia Januari mwaka ujao wawe wameondoa magari yote madogo na kuyahamishia maeneo ya pembezoni ili yaendelee kufanya kazi huko.

Pateli alisema katika kuhakikisha wanaondoa msongamano wa magari katikati ya jiji, LATRA ilianzisha ruti ndefu ambazo zinapitia katikati ya jiji na kwenda maeneo mengine.

Alitoa mfano kuna ruti inayotoka Nyashishi kupitia katikati ya jiji na kuelekea uwanja wa ndege na nyingine zipo za mzunguko kutoka maeneo ya Nysaka kupitia Kona ya Bwiru hadi mjini.

Ofisa huyo wa LATRA alisema wanatarajia wafanyabiashara mbalimbali watajitokeza kununua magari makubwa yanayobeba abiria kuanzia 25 ili waanze kusafirisha abiria katia Jiji la Mwanza.

"Kinacholeta shida hapa ni uwezo wa watu wa Mwanza kuwa mdogo kifedha na hivyo kushindwa kununua magari makubwa ya kusafirisha abiria hapa mjini, tumeishaongea na wamilikia wa magari madogo wanunue magari makubwa, lakini mpaka sasa bado wanasuasua," alisema.

Kwa upande mwingine, LATRA imeonya madereva wa magari ya mikoani wanaokimbia mwendo kasi wakati wa usiku wakidhani muda huo hakuna mtu wa kuwakamata.

Alisema sheria inafanya kazi muda wote na kwamba madereva wanaojidanganya hivyo watakumbana na mkono wa sheria kwa kuwa magari yote yamefungwa vifaa maalum vya kuwafuatilia.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama, akizungumza wakati wa uzinduzi wa wiki ya wawekezaji katika masoko ya mitaji duniani, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mgombea aahidi ujenzi madarasa, madawati

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kibaha Mjini kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Aminata Mshana, amesema endapo atachaguliwa, atasimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa ya kutosha kwenye shule zote ikiwa ni pamoja na uwapo wa madawati.

Aminata alitoa ahadi hiyo juzi alipokuwa katika mkutano wa kampeni Kata ya Mailimoja ambapo alisema akipata ridhaa ya kuwa Mbunge wa Jimbo hilo, atahakikisha hakuna changamoto za elimu upande wa vifaa vya kufundishia na samani zinazohitajika shuleni.

Akizungumzia upande wa afya, alisema, atahakikisha anasimamia huduma za afya bure kwa wanawake, wazee na watoto. Pia ameahidi kila mtaa na kata zote 14 kutakuwapo na wataalamu wa afya wanaozungukia nyumba kwa nyumba kupima afya za wananchi.

Katibu wa ACT-Wazalendo Kata ya Mailimoja, Mussa Hazirun, alisema, kiongozi yeyote akitaka kuongoza anatakiwa kuwapa watoto lishe bora kwanza kama sera ya chama hicho inavyoelekeza kuwaangalia watoto wao.

Naye mgombea udiwani wa chama hicho kata ya Mailimoja, Athumani Lusambi, alisema, endapo wananchi watamchagua ataongea na wadau wa maeneo wasaidie kujenga kituo cha afya na kituo cha polisi katika kata hiyo.

Aidha, Lusambi alisema akichaguliwa kuwa diwani atahakikisha anatumia wahisani katika ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi zilizopo katika kata hiyo.

Aliwasihi wananchi kuhudhuria kwenye mikutano ya kampeni na kusikiliza sera za wagombea na si kubaki nyumbani na kushabikia vyama vya siasa.

Mgombea huyo pia ameahidi kusimamia suala la daladala kuingia katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi kutoka na sasa kuishia katika stendi ya Njuweni wagonjwa na ndugu wanaofika katika hospitali hiyo kulazimika kutumia usafiri wa bajaji na pikipiki.

## AMCOS zatozwa faini mamilioni

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAKALA wa Vipimo Mkoa wa Lindi, umekusanya maduhuli ya Sh. 12,100,000 ikiwa ni malipo ya faini yanayotokana na vyama 22 vya msingi na ushirika (AMCOS) kwa kukutwa na makosa yakiwamo kuchezea mizani na kutumia mawe mazito na yasiyohakikiwa na mamlaka husika.

Meneja wa Wakala wa Vipimo Mkoa, Andrew Mbwambo, aliyaeleza hayo alipokuwa anazungumza na Nipashe na kwamba maduhuli hayo, yamekusanywa kupitia AMCOS 22 kati ya 150, zilizofanyiwa ukaguzi na wataalamu wa vipimo na kukutwa na tatizo hilo, kipindi cha msimu wa mauzo mazao ya korosho na ufuta mwaka 2019/2020.

Mbwambo amefafanua kuwa msimu wa mauzo ya mazao hayo, AMCOS 150 zilizokaguliwa 22 zilikutwa na makosa mbalimbali yakiwamo viongozi na makarani kutokuwa waadilifu, ikiwamo kuharibu mizani kwa makusudi, kutumia mizani na mawe mazito yasiyohakikiwa na mamlaka husika.

Pia, meneja huyo alisema kufuatia vitendo hivyo na wenyewe kukiri makosa husika, Wakala wa Vipimo kupitia Sheria Namba 340 waliwatoza faini ya jumla ya Sh. 12,100,000, ambapo vyama vyote vilivyohusika na makosa vimelipa.

## Mamlaka maji zatakiwa kuwafunda watumishi

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

BODI za Wakurugenzi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira nchini zimetakiwa kuhakikisha watumishi wanaacha tabia ya kuzoea matatizo ya wananchi na badala yake wayatatue kwa wakati.

Hayo yamebainishwa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, wakati akifungua mafunzo ya Bodi za Wakurugenzi na Menejimenti za Mamlaka 14 za Majisafi na Usafi wa Mazingira kutoka Kanda ya Ziwa.

Alisema wajibu wa Bodi za Mamlaka za Maji ni kusimamia shughuli zote za uendeshaji wa mamlaka kwenye utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi, lakini wakati mwingine kumekuwa na malalamiko mbalimbali ikiwamo ya ukosefu wa huduma ya maji ama kero zingine hivyo ni wajibu wa mtumishi kutatua changamoto hiyo na kuachana na tabia waliojijengea ya kuzoea malalamiko hayo.

Alisema lengo la Wizara ya Maji kupitia Mamlaka za Maji kote nchini ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora na toshelevu ya majisafi na salama na kwamba ili kufikia lengo hilo bodi zinapaswa kuwawajibisha watumishi watakaofanya kazi kinyume na utaratibu ikibidi kusimamishwa kazi.

## Waangalizi wote rasmi kazini, wakiwa na mwongozo mkononi

Ukurasa 12





Ukurasa 13

## Wahitaji waomba NEC ijumuishe makamishna wenye ulemavu

siasa

JUMATANO OKTOBA 7, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

UCHAMBUZI

# UKAWA unapojirudisha tena ndani ya mazingira tata ya kuungana

## Viunzi vilivyopo: Kanuni, majina, sheria

**Na Ani Jozeni**

USHIRIKIANO wa vyama vya upinzani ambao haukukamilika kabla ya kuchukua fomu za wagombea kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) Julai mwaka huu, lakini hata ndani ya vyama vya siasa vyenyewe, unaelekea kuibuka tena.

Ni kutokana na mazingira halisi ya kampeni mwezi mmoja tangu shuruba ya kutafuta kura kwa wapigakura kuanza hasa kutokana na kutokuwapo kwa shughuli za wazi za vyama vya siasa tangu uchaguzi mkuu uliopita 2015.

Baada ya hatua ya kwanza ya kampeni kukamilika, vyama vikuu vya upinzani vinaanza kuona kuwa visizongane.

Haikuwa hatua rahisi kufikiwa kwani wagombea walikuwa wameshajiweka 'mguu sawa' katika maeneo mengi na kuambiwa kuwa matayarisho hayo siyo hoja, lazima mustakabali wa uchaguzi uangaliwe upya halikuwa jambo rahisi.

Ilibidi hali yenyewe ijidhihirishe kwa wagombea, viongozi wa vyama na hata wafuasi wao, kuwa kufikia hapo ni kuunganisha nguvu, hata kama kuna vikwazo vilishawekwa katika kanuni za uchaguzi.

Kanuni zinahitaji NEC iarifiwe miezi mitatu kabla ya kuanza kampeni kuwa vyama vitashirikiana, hali ambayo ina maana kuwa ushirikiano huu siyo rasmi.

Ambacho hakipo katika ushirikiano huo mpya ni jina la UKAWA, kwani suala la katiba linatajwa kama mojawapo ya ahadi za wagombea kile kinachoitwa kwa lugha ya uchaguzi kuwa ni 'sera' za wagombea, mojawapo ikiwa ni suala la kukamilisha mchakato wa katiba mpya.

Sera hiyo inakuwa na nguvu zaidi kwa upande wa upinzani kwani wagombea wanaosalia wana hisia zinazofahamika kuhusu mchakato huo, yaani Seif Sharif Hamad wa ACT-Wazalendo kwa upande wa Zanzibar na Tundu Lissu, mgombea urais wa Muungano-(CHADEMA).

Ni wapinzani wakereketwa waliobaki, tofauti na mchujo 2015 ambako aliyehamia CHADEMA kutoka CCM alibeba bendera ya wapinzani wengi.

Kutokana na upya ndani ya upinzani, mgombea wa ACT-Wazalendo Bernard Membe, asingeweza kuwaunganisha kwa kina watetezi wa katiba mpya kwa vile hakuwepo wakati wa UKAWA ila mwelekeo wake binafsi ungebadilishwa na kuingia katika mtizamo tofauti wa kisiasa.

Aliingia ACT-Wazalendo kama Edward Lowassa alivyofanya uchaguzi mkuu uliopita lakini mazingira yake yalikuwa tofauti, kwani hayakutanguliwa na ushindani wa 'kukata na shoka'.

Hali ya kutoridhishwa na uteuzi peke yake haikumzuia kufanya kampeni. Hata hivyo kinachojiri sasa kwa uteuzi wa mwana CCM mwenziwe Membe waliokuwa wote kuwania nafasi ya urais 2015 bado yanatofautiana.

Yako mazingira ya ziada ambako ingekuwa vigumu hata hivyo kwa CHADEMA kujiaminisha kuwa inafanya kampeni ya dhati ya kupata kiti cha urais kwa upande wa Zanzibar, wakati ambapo ACT-Wazalendo, 'kila kitu kingebaki sawa'.

Chama hicho kilikuwa na uwezo kama CHADEMA wa kufanya kampeni kwa kiti cha urais upande wa Muungano. Ndiyo hapo mazingira ya ziada yakaanza kujionyesha, ambayo msingi wake ni tofauti ya 'njia waliyopitia' wagombea hao wawili wa urais Muungano; ni vigezo vipi vya kugombea vinavutia wananchi? Lissu alikuwa na nafasi na nguvu ya ushawishi zaidi wa kisiasa ikilinganishwa na Membe.

Kimsingi tofauti kubwa kati yao ni historia walizokuwa nazo ndani ya miaka mitano iliyopita mbele ya wapigakura na wafuasi wao, walishasikia mengi zaidi yanayomhusu Lissu.

Kila mahali umma huo wa kisiasa ulikuwa una shauku ya kumwona, kumsikia na kumfuatilia mwanasheria machachari, kimsingi ndiyo mazingira yanayombeba kisiasa.

Ni mazingira yanayompatia Lissu ushujaa mbele ya wapigakura ukiwa umejengwa na hulka yake, ambao mfumo wake una historoa mathalani kwa wanasiasa kama Nelson Mandela wa Afrika Kusini.

Pale, Lissu anapojitokeza kama lulu mbele ya wapigakura wake, kutaka kujua ni nani huyu aliyefunika mawimbi katika anga za siasa na kuwa kielelezo cha kipekee kuchambua hali ya siasa nchini.

Haikuwa hapa suala la sera ila mtu maalum mwenye historia maalum zaidi. Nadharia hiyo, pia ipo katika sayansia ya siasa inayoelezea njia kuu mbili zinazomnadi mwanasiasa;

Chama na sera zake na wasifu binafsi wa mwanasiasa.

Katika hilo la umaarufu Membe alikuwa na kete pungufu ikiwamo kufahamika kwa kina mbele ya wapigakura wake kama alivyo Lissu.

Unaweza kusema kuwa umaarufu wa Membe kwa takribani miaka iliyopita, zaidi ulikuwa katika mitandao, ambayo ni wachache waliokuwa wakimfuatilia na matukio yaliyomhusu.

Ni kile Waingereza wanachokiita 'a storm in a tea cup' ikimaanisha dhoruba katika kikombe cha chai haibadili lolote katika kile wapigakura wanachofahamu.

Hivyo ushirikiano mpya wa vyama vya siasa kimsingi umelazimishwa na mazingira halisi yanayojiri katika kampeni kuwa CHADEMA haina mizizi ya kutosha Zanzibar kufanya yanayolingana na hadhi ya chama hicho kitaifa.

ACT-Wazalendo kwa upande wake, ilizidiwa na umaarufu wa mgombea urais wa Muungano CHADEMA, hata hivyo haitakuwa rahisi kwa vyama hivyo kuhakikisha kuwa wapigakura wao wanaendana na maelekezo yao.

Hiyo ni katika mtazamo wa kuhakikisha wanamuunga mkono mgombea mwenye uwezo zaidi wa kushinda katika nafasi za ubunge na udiwani kulingana na wasifu wa aliyepo.



Membe alipo kabidhiwa fomu za kugombea urais wa Muungano kwa tiketi ya ACT-Wazalendo.**PICHA: MTANDAO.**

JOTO UCHAGUZI MKUU:

# Waangalizi wote rasmi kazini, wakiwa na mwongozo mkononi

## • Nao wanena walio nayo kwa sasa

**Na Christina Mwakangale**

ZIMEBAKI siku 21 kufikia ile ya kupiga kura, Jumatano ya Oktoba 28, umma wa wapigakura utakapoingia kwenye vyumba husika walikopangiwa, kushiriki tendo hilo la kihistoria na uamuzi mkuu.

Hilo lipo, huku jamii ikiendelea kuhitaji ufahamu wa mwenendo mzima wa mchakato wa kuwachagua viongozi, ambayo ni elimu ya uchaguzi.

Inawezekana wapo wanaoweza kuhisi kuwa elimu ya uchaguzi ni kama marudio kwa walioshiriki uchaguzi uliopita. Ila, ukweli kuna mengi zaidi ya hapo.

Ikumbukwe, mathalan kuna kundi kubwa la vijana walioingia umri rasmi wa kupiga kura baada ya kutimiza miaka 18. Ni wageni na hawakuwapo kwenye uchaguzi uliopita, hivyo wanahitaji elimu hiyo.

Pamoja na hao, wapo wengi ambao wangependa kujua ya kisheria kuhusu uchaguzi, ikiwamo taratibu na kanuni zinazotolewa ufafanuzi na wanasheria, wabobezi na wasomi wa uchaguzi kikanda na kimataifa, ili kuleta uelewa miongoni mwa jamii.



Namna ilivyokuwa upigaji kura na uangalizi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. **PICHA: MTANDAO.**

**NENO LA MWANGALIZI**

Deus Kibamba, ni kati ya Mtanzania mwangalizi anayeshiriki sana kufuatilia mchakato huo ndani na nje ya nchi hususan barani Afrika, katika miaka ya hivi karibuni.

Anasema, uzoefu wa kushiriki kwenye michakato ya uchaguzi mbalimbali, ikiwamo ya kikanda, unaonyesha kila unapofika uchaguzi mkuu kunakuwapo mambo mapya au yaliyopo kisheria, jamii inahitaji kufahamishwa, ili kuyazingatia wakati wanapokwenda kupigakura.

Kibamba anataja muhimu kwa ajili ya uchaguzi huo mkuu, unawahusi waangalizi wa nje na ndani na mwaka huu, Tanzania itakuwa na waangalizi 15 kushuhudia, hivyo ni suala linalohitaji kufahamika na wengi.

"Waangalizi wapo wa aina mbili wa ndani na wa nje. Ni wageni kutoka nchi ambazo hutuma watu wake kufuatilia mchakato wote wa uchaguzi kwa vibali maalum.

"Waangalizi wa ndani ni wale ambao hutoka kwenye makundi mbalimbali ya ndani ya nchi vikiwamo, vyama vya siasa, asasi za kiraia na taasisi za elimu kushuhudia uchaguzi," anaeleza Kibamba.

Anaeleza majukumu ya waangalizi wa uchaguzi hutofautiana na iwapo ni mwangalizi wa nje au ndani, baadhi yao huanza kazi mapema miezi miwili au mitatu kabla, kulingana na walivyojipanga na maelekezo ya vibali vyao.

Kibamba anasema waangalizi wa uchaguzi kutoka nje, kazi yao kubwa ushuhuda wa macho zaidi na kila wanaloliona ambalo pengine hawakuridhika au wanashuhudia ni kikwazo wanaliweka katika kumbukumbu.

"Kama ni mwangalizi wa ndani iwapo kuna jambo umeona limejitokeza, unaweza ukatoa ushauri. Waangalizi ni tofauti kabisa na wasimamizi wa uchaguzi," anasema.

Pia, anasema hawaruhusiwi na kanuni kuingilia mchakato wa uchaguzi uliokwishaandaliwa, bali kazi yao ni kuangalia au kurekodi mwenendo wa uchaguzi na kukabidhi ripoti kwa wahusika, ikiwao Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na vyombo vinginevyo.

Kibamba anasema waangalizi wa uchaguzi huomba vibali maalumu kutoka nchi husika wanakosimamia uchaguzi na nchini, NEC ndiyo inayohusika kuvitoa.

Pia, anafafanua kwamba, waangalizi ama wanafahamishwa au kutambulishwa kwa umma na muda wote wa kazi zao huvaa vitambulisho, magari wanayoyatumia huwekewa mabango yanayowatambulisha.

"Waangalizi hupaswa kuvaa makoti, kofia, vitambulisho ili kutambulishwa. Kusema wewe mfano ni mwangalizi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki, ni lazima ujulikane. Usipojulikana unaweza ukadhaniwa unataka kuchukua habari, lazima utambulike," anaeleza Kibamba.

**KUTOKA NEC**

Emmanuel Kawishe, ni Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi, anayesema waangalizi au watazamaji wa uchaguzi wa ndani na nje, hupewa mwongozo na tume hiyo, kuhusu maeneo wanayohitajika kwenda.

Anakumbusha kuwa, waangalizi hao hawaruhusiwi kuingilia mchakato wa uchaguzi, zaidi ya kutoa maoni kwa maandishi kile wanachokiona iwapo kilikwenda tofauti na kanuni zilizoko.

"Tume inawapa orodha ya vyama vilivyosajiliwa na vinavyoshiriki uchaguzi, ramani za majimbo. Uchaguzi ni suala la kitaifa linahitaji sheria na kanuni," anasema.

Kiongozi huyo wa NEC anaendelea: "Kama mtu hajachaguliwa kutazama haruhusiwi kutazama mwendendo wa uchaguzi."

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, mnamo Juni mwaka huu alieleza kutolewa vibali kwa asasi 27 nchini kuwa waangalizi wa ndani huku ikitoa vibali kwa asasi 245 kutoa elimu ya mpigakura.

Dk. Mahera anasema, jumla ya nchi 15 ziliwasilisha maombi, kufanya uangalizi katika uchaguzi mkuu ujao na wiki iliyopita ziliruhusiwa.

**WIZARA YA NJE**

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imewaagiza waangalizi hao kufanya vipimo vya virusi vya corona, kabla ya kuingia nchini.

Profesa Palamagamba Kabudi, anasema nchi hizo zilishafuata taratibu za maombi na kupata kibali cha uangalizi wa uchaguzi kupitia balozi zao zilizopo nchini baada ya NEC kufungua maombi kwa waangalizi wa kimataifa.

Katika mazungumzo yake na Manfred Fanti, Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU), Profesa Kabudi amethibitisha kuwa mataifa 15 yamesharuhusiwa kupeleka waangalizi kufuatilia uchaguzi.

Sheria zilizopo zina mwongozo kimataifa na zinaruhusu waangalizi wa kimataifa na anasema, hadi sasa kuna jumla ya mataifa 15 yaliyoruhusiwa kufanya uangalizi wa uchaguzi mkuu, yote yakiwamo makubwa ya Magharibi; Ufaransa, Uingereza, Hispania na Ubelgiji.

Profesa Kabudi anasema, waangalizi hao watalazimika kuhakikisha wanapima afya zao dhidi ya virusi vya corona na kwamba waangalizi watakaokwenda Zanzibar wawasilishe maombi yao kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Balozi wa EU, anasema umoja huo utafuatilia mchakato wa kampeni za uchaguzi mkuu zinavyoendelea na hadi sasa ameleza kukiri kuridhishwa na nazo, kwamba zipo kwa uhuru na amani na hatua waliopo sasa, wanajiandaa na uangalizi.

Wakati waangalizi hao wa kimataifa wakipata kibali cha uangalizi, NEC inasema itaunda kamati maalumu itakayoratibu mwenendo wa waangalizi hao wa uchaguzi, ili wasikiuke miongozo waliopewa kisheria na kanuni.


Deous Kibamba akizungumza katika majukwaa ya kisiasa. **PICHA :MTANDAO.**

# Wahitaji waomba NEC ijumuishe makamishna wenye ulemavu

## •Wajengewe makazi maalumu



Noel Gumbo (kushoto) na Rehema Kingu'ng'aro wakizungumzia changamoto za wahitaji kwenye ushiriki uchaguzi na haja ya makazi bora. **PICHA: MWANDISHI WETU.**

**Na Gaudensia Mngumi**

WAKATI kampeni za uchaguzi zikipamba moto na serikali ya awamu ya tano ikijinadi kimafanikio kama kugharamia masomo ya msingi hadi sekondari , kujenga reli ya kisasa (SGR) na ujenzi wa ukuta wa tanzanite Mererani, wenye ulemavu wanazipongeza hatua hizo, lakini 'wana jambo lao'

Ombi lao kwa serikali ni kuacha alama ya kipekee kwao kwa kuwajengea makazi au kijiji cha wahitaji ili uwe urithi usiofutika kama ilivyo SGR, daraja ya baharini na ukuta wa Mererani.

Wanaiomba iwajengee na kuwaachia makazi maalumu ya wahitaji yatakayojulikana kama kijiji cha wenye uhitaji maalumu, katika miji na majiji ya Mwanza, Arusha, Dodoma na Dar es Salaam.

Wanasema hayo kwenye mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam, kuhusu hatima yao kwenye mchakato wa kutiania na kuteuliwa wagombea kwenye uchaguzi mkuu.

Rehema Kingu'ng'aro Mkurugenzi wa Shirika la Kitaifa la Wenye Ulemavu (TNDA), anasema wenye ulemavu wengi hawana nyumba, makazi bora na maisha yao ni duni na hata wanapopewa viwanja inakuwa vigumu kujenga kwa sababu ya kukosa kipato hivyo kushindwa kununua vifaa vya ujenzi.

Anasema makazi maalumu ni muhimu kwa kuwa yatakuwa na miundombinu rafiki kama ngazi, lift, sehemu za kufanyia biashara, huduma za jamii hasa vyoo, mahali za kunawa mikono na hata mabafu kwa ajili ya wahitaji hao.

Wenye ulemavu wengi hawana kipato hivyo hata makazi yao ni changamoto lakini pia wanaathiriwa na unyanyapaa na miundombonu isiyo rafiki kwenye maeneo wanayopanga na ufumbuzi wa tatizo hilo ni serikali kuweka makazi ya kiupendeleo kwa wahitaji, anasema.

Anaeleza kuwa hata kama watalazimika kuchangia garama wanaomba iwe kidogo ili waweze kuzimudu.

### MAKAMISHANA WALEMAVU

Rehema akizungumzia ushiriki kwenye ubunge kwa viti maalumu anasema baada ya mchujo na kupata wagombea miongoni mwa watiania wakiwamo wenye ulemavu, wahusika kwenye kundi hilo wana mengi ya kuishauri serikali.

"Tunaamini kuwa endapo changamoto kadhaa zinazojitokeza kila mara wakati wa kushiriki mchakato wa kuchuja watiania ili kupata wagombea zitafanyiwa kazi tutakuwa na mafanikio zaidi na pengine kutakuwa na ushindani zaidi miongoni mwetu,"anashauri Rehema.

Mkurugenzi wa Shirika la Kitaifa la Wenye Ulemavu ambaye pia ni mwalimu wa Sekondari ya Pugu, mkoani Pwani, anaeleza kuwa mambo yanakuwa magumu kwa wenye elemavu kupata fursa kikamilifu kutokana na kutokushirikishwa katika mipango na maamuzi yanayofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kwenye kupanga mambo yanayowahusu.

"Tunaomba pia katika uteuzi wa makamishna NEC serikali ifikirie kuwajumuisha wenye ulemavu ili wawakilishe mahitaji, hali na jinsi ya kuishi na ulemavu ilivyo hasa wanapofanya maamuzi kuhusu kundi hili kwenye masuala yote yanayohusu uchaguzi" anashauri Rehema.

Anaamini kuwa wakiwamo makamishna wenye uhitaji maalumu kama kiziwi, bubu, wasiona, ulemavu wa viungo au mchanganyiko atakuwa katika nafasi nzuri kuwazungumzia wanaoishi na changamoto.

### UWEZESHAJI

Rehema anasema kiuchumi wenye ulemavu hawajiwezi si rahisi waonyeshania wenye uhitaji wakaweza kujigharamia na kuwagharamia wasaidizi wao hivyo, wanaoimba NEC inapoandaa mchakato huo iwawezeshe kikamilifu kwa hatua zote.

"Tunaomba kuwe na miundombinu rafiki ukumbini tunapojinadi, uwepo usafiri, malazi na pia kuwagharamia wasindikizaji wetu. Kwa mfano mimi nisiyeona nijajigharamia pamoja na kumlipia msaidizi wangu anayenishika mkono na kunisaidia kutembea. NEC ijue kuwa tunapata gharama mara mbili. Ni vigumu hili nalo tunaomba tume iweke bajeti," anashauri Rehema.

Suala jingine analoishauri tume ni kuweka utaratibu wa kuwasafirisha, kulala na kuwafikisha ukumbini pamoja na kuwarudisha hotelini hadi makwao badala ya kuwaachia mzigo huo peke yao kwa kuwa wanaitwa 'spesho ' kwa maana ya uhitaji maalumu hata kile kinachofanyika pia kiwe 'spesho'.

Rehema anasema kwa mfano walikuwa watiania 18 Dar es Salaam kwa upande wa vitimaalumu wakati wasioona walikuwa wanne na kwamba NEC ingeweza kuwa na namna bora zaidi ya kuwahudumia."Si hivyo tu hata kututoza Sh. 100,000 kwa fomu ni changamoto. Wanaoishi na ulemavu wengi ni maskini. Kusema mlemavu ajitegemee usafiri, malazi na kulipia fomu ni gharama kubwa. Tunaomba watufikirie na kutuondolea pesa ya fomu au kutupunguzia hata iwe 10,000. "

Anazungumzia kukosekana lugha maalumu kwa wasioona anasema namba walizokuwa wanazitumia kuomba kura ziliandikwa kwa tarakimu za kawaida hivyo kushindwa kuzisoma.

Anaeleza kuwa wahitaji walitakiwa kuwekewa lebo ya brail. (maandishi ya nukta nundu) ili wazisome na kuwaelekezea wapiga kura.

### KUPATIWA 'MENTORS'

Katibu Mtendaji wa Shirika la Kitaifa la Wenye Ulemavu, Noel Gumbo, anasema wanawake wagombea uongozi wanahitaji 'mentors' kwa ajili ya kuwafundisha mambo yalivyo kwenye jukumu wanaloliendea na pia 'mentors' kujifunza kutoka kwa wahitaji hao.

"Wanatakiwa kuelezwa kuhusu mazingira ya ukumbi, utaratibu, vifaa, ratiba na hali halisi wanayoiendea kuliko kuachwa wakae bila kuwa na wazo la kile kitakachokwenda kutokea.

### KUPEANA MREJESHO

Gumbo anatamani kuwe na mrejesho baada ya mchakato wa kusaka watiania mahususi kwa walemavu ili wajue wakati wa kutafuta wagombea walikosea wapi, walifanya vizuri eneo gani na nini wafanye ili kurekebisha kasoro na kufaulu zaidi siku za usoni, badala ya kukaa kimya bila wenye mahitaji kujua kasoro na upungufu wao.

### MAFUNZO MAALUMU

Katibu Mtendaji Gumbo, anapozungumzia mchakato huo anasema ni vyema kuwafundisha viongozi na wagombea wenye uhitaji masuala ya maadili kwani hakuna mtu wa kuwaeleza kuhusu maadili na namna ya kutekeleza majukumu katika utaratibu unaokubalika.

"Unaweza kusikia walemavu wanahasira sana, hawana uvumilifu. Hawajiamini ni vigumu kufanya nao kazi, siyo vizuri", anasema Gumbo na kuongeza kuwa yote hayo yanaweza kuondoka iwapo watafunzwa na kupewa mafunzo maalumu ya maadili na uongozi mara kwa mara badala ya kuchwa kama walivyo.

Anakumbusha kuwa ni vigumu kwao kujiongeza na kujipa utaalamu zaidi kwa vile hakuna kitabu, majarida wala mafunzo kwenye ulemavu yanayoweza kuongeza na kukuza ujuzi, mathalani wasioona hakuna vitabu vyenye maandishi ya nukta nundu au brail.

"Tukishaondoka shuleni ndiyo tumeacha kila kitu. Huku hakuna maktaba, magazeti, wala vitabu na majarida ya maandishi ya nukta nundu kwa wasioona. Ndiyo maana tunatakiwa kufunzwa miiko, halihalisi, taratibu pamoja na maadili kama viongozi wa jamii ili tufanyekazi katika mazingira ya kukubalika na kueleweka na jamii," anasisitiza Gumbo.

### MABADILIKO KIKATIBA

Gumbo anazungumzia kuboresha katiba na kubadilisha utaratibu wa uteuzi wa wabunge viti maalum ili uhusishe wanaume wenye ulemavu.

Anaongeza kuwa kuna haja ya kuwaweka pia wanaume wanaoishi na ulemavu kuwa wabunge wa viti maalumu kama inavyofanyika kwa wanawake.

"Tunahitaji kuona kundi la wabunge alibino, wenye ulemavu wa kusikia, wasioona, bubu viziwi, viungo na wenye ulemavu wa akili wakiteuliwa kwenye viti maalumu." Anasema Gumbo na kuongeza kuwa wenye ulemavu wa akili wabunge wao wanatokana na wazazi au walezi wao ambao humchagua mwakilishi wao.

## IBRAHIM BOUBACAR KEITA

# MZANDIKI, MFUASI WA SIASA ZA KUNG'ANG'ANIA MADARAKA ALIYEFURUSHWA IKULU NA WANAJESHI



Rais wa zamani wa Mali Ibrahim Boubacar Keita,

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa zamani wa Mali Ibrahim Boubacar Keita, ni miongoni mwa viongozi Afika wanaoonja joto la kukataliwa na umma wanaong'ang'ania kuuongoza.

Kiongozi huyo, amejiponza mwenyewe kwa kuendeleza siasa za kibabe, kutojali sauti ya umma na kuona kuwa maslahi binafsi ni muhimu kuliko kuondoka ikulu, akijidanganya kuwa hakuna atakayeweza kuongoza Mali ila yeye.

Kiongozi huyo aliyezaliwa Januari 29 1945, alikuwa akijulikana kwa kifupi kama IBK, ameliongoza taifa hilo la Mali kuanzia Septemba 2013 hadi Agosti 2020, alipolazimishwa na jeshi kuondoka ikulu pamoja na Waziri Mkuu Boubou Cisse.

Anapinduliwa kwa sababu ya ufisadi, kung'ang'ania madaraka na kuendeleza ubabe hata pale anapoona kuwa hatakiwi.

Ibrahim Boubacar Keïta (IBK), awali alikuwa Waziri Mkuu kuanzia mwaka 1994 hadi mwaka 2000. Katika kipindi cha kuanzia 2002 hadi 2007 alikuwa Rais wa Bunge la Mali. Ilipofika mwaka 2001 alianzisha chama cha kisiasa cha Rally for Mali (RPM). Hakufanya ajizi akagombea urais na Julai 2013, alichaguliwa kuwa rais na ilipofika Septemba 4, 2013 aliapishwa na kuchukua uongozi.

Utumishi wa miaka saba kuwatumikia watu wa Mali ulikoma Agosti 2020, alipolazimika kutangaza kujiuzulu kupitia televisheni ya taifa baada ya wanajeshi waasi kumkamata pamoja na Waziri wake mkuu Boubou Cisse, katika mapinduzi yaliyotokea mji mkuu wa Bamako.

Wakati anatangaza azma ya kung'atuka Keita alisema kujiuzulu kwake kunaanza mara moja hatua iliyoonekana kuwa ni ya kushinikizwa kwani picha za video zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha msafara ulioaminika kuwa wa Keita na Cisse uliokuwa umezingirwa na wanajeshi.

Baada ya kupita siku 10 tangu yalipotokea mapinduzi, wanajeshi walimteua Kanali aliyeongoza mapinduzi hayo, Assimi Goita, kuwa rais mpya wa nchi hiyo.

Kabla ya wanajeshi kumteua kuwa Rais wa Mali, Kanali Assimi Goita, alikuwa Mkuu wa Kamati ya Taifa ya Kijeshi ya nchi hiyo iliyoundwa baada ya kupinduliwa Rais Boubacar Keïta.

### KILICHOMTOA IKULU

Rais Keita alipinduliwa Agosti, 18 kufuatia maandamano makubwa dhidi ya serikali yake akituhumiwa kwa ufisadi , usimamizi mbaya uchumi na pia kudaiwa kusababisha mgogoro kuhusu matokeo ya uchaguzi wa ubunge nchini humo.

Licha ya kuwapo machafuko na migogoro iliyoitesa Mali kwa miaka mingi sasa, lakini katika miezi ya hivi karibuni kulikuwa na maandamano makubwa huku vyama vya upinzani vikitaka Rais Boubacar Keïta ang'oke madarakani. Pamoja na hayo Keita aliendelea kung'ang'ania madaraka na kupelekea kuongezeka mgogoro wa kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Licha ya mapinduzi hayo kusababisha shutuma za kimataifa ikiwamo Umoja wa Afrika (AU) Jumuiya ya kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS), Umoja wa Mataifa (UN), Ufaransa, Umoja wa Ulaya (EU) kote wamelaani uasi huo na kuonya juu ya jaribio lolote la kubadili madaraka kinyume na katiba katika taifa hilo.

Lakini, maasi yanaungwa mkono na raia wa Mali na wanajeshi ambao walimkamata Keita lakini pia aliachiwa.

IBK mwenye miaka 75, mapema mwezi uliopita alipelekwa Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kutibiwa baada ya kupata kiharusi maelezo yaliyotolewa na maofisa wa jeshi. Anadaiwa kupata tatizo la 'ischaemic attack' ambalo ni matokeo ya kukosekana damu ya kutosha ubongoni unaosababisha sehemu nyingine kukosa hewa safi na chakula.

Jeshi baada ya kuchukua nchi lilianza mazungumzo na upinzani na makundi ya asasi za kiraia kuhusu utawala wa mpito wa kiraia, hata hivyo lilisema kuwa litaondoka madarakani ndani ya miaka miwili lakini viongozi wa Afrika Magharibi wanataka makabidhiano ya madaraka yafanyike kwa haraka.

> Tangu Agosti 18, tunazungumza kuhusu historia ya taifa letu," Kiongozi wa pili wa wanajeshi waasi Malick Diaw , alizungumza kwenye ufunguzi wa mazungumzo hayo, na shirika la AFP likaripoti.

Viongozi wa mapinduzi wameahidi kuheshimu makubaliano ya kimataifa katika kupambana na wanamgambo. Maelfu ya vikosi vya Ufaransa, Afrika na Umoja wa Mataifa vimekita kambi nchini Mali kupambana na wanamgambo.

Aidha, zaidi ya wawakilishi 500 wa upinzani nchini humo na makundi ya asasi za kiraia wanafanya mazungumzo na wanajeshi waliompindua Keita mjini Bamako wakijadili masuala ya utawala wa kiraia.

"Tangu Agosti 18, tunazungumza kuhusu historia ya taifa letu," Kiongozi wa pili wa wanajeshi waasi Malick Diaw , alizungumza kwenye ufunguzi wa mazungumzo hayo, na shirika la AFP likaripoti.

Katika jitihada za kuweka mazingira bora ya kidemokrasia mazungumzo yalipangwa kuendelea mpaka katikati ya Septemba.

### TAIFA LA MAPINDUZI

Keita au IBK si wa kwanza kupinduliwa, taifa hilo lina historia ya kupinduana na itakumbukwa kuwa Novemba 19, 1968 mapinduzi mengine yasiyomwaga damu yalimuondoa madarakani Rais Modibo Keïta. Kiongozi wa mapinduzi hayo alikuwa Meja Jenerali Moussa Traore ambaye baadaye alikuwa rais wa taifa hilo.

Machi 26, 1991 yalifanyika mapinduzi ya kumuondoa Traore madarakani baada ya miongo miwili ya kidikteta ya kuutawala mali. Japo mwaka 1968, Traoré aliongoza mapinduzi, msemo wa mwosha huoshwa ulimfika baada ya kumuondoa Modibo Keïta na kujitangazia kuwa rais wa pili wa Mali.

Luteni Kanali Amadou Toumani Touré, ndiye kiongozi wa mapinduzi yaliyomng'oa Traoré madarakani , katika sakata ambalo liliuawa watu wengine na maofisa wa jeshi zaidi ya 59 na wengine 200 walijeruhiwa maujia yaliyohusisha kulipa kisasa. Kaka wa Troure aliyekuwa Waziri wa Elimu Bakary Traore na Mamadou Diarra, aliyekuwa shemeji yake waliochomwa moto hadi kufa.

Rais wa zamani Moussa Traoré, alitupwa gerezani kuanzia mwaka 1992 baada ya kuhukumiwa kifo myeye pamoja na mkewe , lakini rais wa Mali Alpha Oumar Konaré, alibadilisha hukumu hiyo na kuifanya kuwa kifungo cha maisha jela na alipoondoka madarakani Mei 2002, Konaré aliwasamehe.Alpha Oumar Konaré aliiongoza Mali kuanzia 1992 hadi 2002.

**MITANDAO**



# Wakazi wagoma kutoa maeneo yao

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WAKAZI wa Msalato jijini Dodoma, wameigomea Halmashauri ya Jiji hilo, kuchukua maeneo yao kwa ajili ya kuwapatia wawekezaji bila kuwashirikisha.

Kutokana na hali hiyo, wamesema endapo wataendelea kulazimishwa watawashtaki kwa Rais John Magufuli.

Wakizungumza kwa niaba ya wananchi wenzake kwenye mkutano baina yao na wataalamu wa masuala ya ardhi na uwekezaji kupitia Mpango Kabambe wa Mamlaka ya Uwekezaji wa Kanda Maalum (EPZA), Frank Betwel, alisema hawatakubali hata mara moja jiji hilo kuchukua ardhi yao na kuwapatia wawekezaji bila wao kushirikishwa.

Betwel alisema wanachotaka wao ni kupimiwa na kurasimishiwa maeneo yao ili wao ndiyo wawauzie maeneo ardhi wawekezaji.

"Hapa kinachoonekana ni kuwa kuna kautapeli kanaendelea kwanini jiji walazimishe wao kuchukua maeneo yetu, ili kuwapa wawekezaji badala ya wao kutupimia maeneo yetu ili sisi wenyewe ndiyo tuwauzie maeneo yetu hao wawekezaji," alisema.

Naye Philipo Mahende alisema hawataruhusu hali hiyo itokee kama uongozi wa jiji hautafuata utaratibu wa kutwaa ardhi ikiwamo ulipaji wa fidia.

"Maeneo yetu yamekuwa yakichukuliwa kila mara. Walikuja watu wa uwanja wa ndege tumefanyiwa tathmini, lakini mpaka sasa hatujalipwa hata shilingi moja na leo hii wanakuja tena watu wa EPZA wanataka kuchukua maeneo yetu kwa ajili ya uwekezaji bila hata kutushirikisha wananchi," alisema.

Mahende alisema kama uongozi wa jiji hautakubaliana na maamuzi yao ya kupimiwa maeneo yao na kupatiwa hati miliki, ili wayauze wenyewe kwa wawekezaji, wako tayari kumuona Rais Magufuli na kumfikishia kilio chao.

Sheikh wa Msikiti wa Msalato, Aboubakary Omary, alisema hali hiyo inatokana na uongozi wa jiji kutowajibika kwa wananchi kwa mujibu wa sheria.

"Viongozi wa jiji wanadharau sana wananchi ndiyo maana kila mara mkurugenzi wa jiji haji kwenye mikutano, anatuma wawakilishi ambao hawana majibu kwetu kila siku tunapoteza muda kuja katika mikutano kama hii bila kupatiwa ufumbuzi wa malalamiko yetu," alisema.

Pia alisema kama viongozi wa jiji hawataki kuja katika mikutano na kujibu malalamiko ya wanachi basi mwenyekiti hatakiwi kuitisha mkutano.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Msalato, Emmanuel Mazengo, alisema amekuwa akimwalika Mkurugenzi wa Jiji kila anapoitisha mikutano kwa ajili ya wananchi kupatiwa taarifa mbalimbali, lakini amekuwa hafiki.

"Nimekuwa nikipeleka barua za kumwalika mkurugenzi na kumsainisha ili afike kwenye mikutano yetu lakini hafiki na mimi siwezi kumfunga kamba ili aje kujibu hoja za wananchi," alisema Mazengo.

# Maaskofu waitaka NEC kutenda haki

**Na Peter Mkwavila**, DODOMA

CHAMA cha Maaskofu na Wachungaji (TPA), kimeiomba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kusimamia uchaguzi mkuu kwa kuzingatia miongozo na kanuni, ili kuondoa malalamiko ambayo yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara.

Rais wa chama hicho, Askofu Musa Mlawi, alitoa ombi hilo alipokuwa akizungumza na waumini kutoka madhehebu mbalimbali ya dini kwenye kongamano la kitaifa la maombi lililofanyika jijini hapa.

Askofu Mlawi alisema Watanzania wengi wana imani na tume hiyo kwamba inasimamia haki na kufuata miongozo na kanuni, hivyo ihakikishe inatenda haki kwa kila chama.

**Huu uchaguzi utakuwa huru na haki hata kama kuna dosari ndogo ndogo za kiutendaji zinazojitokeza.**

"Huu uchaguzi utakuwa huru na haki hata kama kuna dosari ndogo ndogo za kiutendaji zinazojitokeza," alisema.

Alisema chama hicho kinaamini kwa asilimia zote kuwa uchaguzi huo utakuwa huru na wa haki kutokana na Watanzania wengi kuwa waaminifu.

"Watanzania ni waaminifu wameombea uchaguzi huu ikiwamo na kuiombea Tume, chama hiki kinaamini utafanyika kwa misingi na kanuni zote na Taifa litawapata viongozi ambao ni chaguo la Mungu mwenyewe," alisema.

Pia aliwataka Watanzania wenye vitambulisho vya kupigia kura, kutimiza haki yao ya kimsingi kwa kujitokeza ili wachague viongozi watakaowaletea maendeleo.

Kongamano hilo la maombi ambalo lilijumuisha watu mbalimbali kutoka madhehebu yote ya dini, liliambatana na ufunguzi wa baraka kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu uliopangwa kufanyika Oktoba 28, ili upite katika hali ya utulivu na amani kubwa.

Aidha, aliwataka Watanzania kuhakikisha wanajitokeza kupiga kura na kumchagua kiongozi bora atakayeongoza nchi kwa miaka mingine mitano.

Katika hatua nyingine, aliwataka wagombea mbalimbali wa nafasi zote za urais, ubunge na udiwani, kutumia mikutano ya kampeni kunadi sera za vyama vyao na kuacha kutumia lugha za matusi au kuchafuana.



Vijana wakisaka wateja wa nyasi za kulisha mifugo katika eneo la Jamatini, jijini Dodoma jana, ambapo toroli moja la nyasi linauzwa kwa bei ya 3,000/-. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Serikali yaahidi kuendelea kuwajali walimu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amesema, serikali itaendelea kuwajali walimu na kuwataka kuchapa kazi ili kukuza elimu nchini.

Pia amesema serikali imeboresha vyuo vitano nchini kwa ajili ya kutoa wataalamu wabobezi katika sekta mbalimbali muhimu.

Mhagama aliyasema hayo juzi kwenye kongamano la walimu lililoandaliwa na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) jijini hapa.

Alisema serikali kwa kutambua mchango unaotolewa na walimu, imefanya mambo mbalimbali ikiwamo kuboresha mazingira ya kufundishia ili kufanya kazi.

Kuhusu vyuo hivyo, Mhagama alitaja miongoni mwa vyuo hivyo kuwa ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kwa ajili ya mambo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), Chuo cha Teknolojia Mwanza kwa ajili ya kutoa wataalamu wa ngozi, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kutoa wabobezi wa usafiri wa anga na Chuo cha Ufundi cha Arusha (ATC) kwa ajili ya wabobezi kwenye nishati.

"Lengo letu ni kuona elimu inakuwa juu kwa wanafunzi. Tunahitaji kuona wabobezi katika taaluma mbalimbali," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali imetoa kompyuta 1,550 kwa ajili ya kuwafundisha walimu masuala ya TEHAMA.

Alisema wameamua kufanya hivyo ili kuhakikisha walimu wanaboresha ufundishaji wao kulingana na matumizi ya teknolojia.

Aidha, alisema serikali itaendelea kufanyia kazi suala la upandishaji madaraja kwa wale wanaostahili.

Waziri huyo aliwatoa hofu walimu kwamba serikali itaendelea kuboresha mazingira yao ya kufanyia kazi na pia kwa kuongeza nafasi za ajira kwa walimu.

"Walimu msiwe na wasiwasi serikali ipo pamoja na nyinyi masuala yenu inayaangalia kwa karibu," alisema Mhagama.

Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, alisema walimu wana imani na serikali, hivyo hawatamwangusha Rais John Magufuli katika mambo ya maendeleo anayofanya.

Naye Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema pamoja na walimu kupandishwa madaraja, bado wanaomba serikali kuendelea kupandisha walimu wengine ambao wanastaili kufanyiwa hivyo.

Ulaya alisema serikali imetoa agizo la kupandishwa madaraja, lakini kuna ucheleweshwaji wa zoezi hilo.





# Waomba madarasa kwa wenye uhitaji maalumu

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

WALIMU wa Shule ya Msingi Mwenge, Kyela mkoani Mbeya, wameendelea kuikumbusha serikali kujenga vyumba vitano vya madarasa kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe juzi, Mwalimu wa Kitengo cha Huduma kwa Watoto wenye Mahitaji Maalum, Benjamini Mwansombelo, alisema watoto wanaofikia hatua nzuri ya uelewa darasani, wanalazimika kurudi nyuma kwa sababu ya uhaba wa vyumba vya madarasa.

Mwansombelo alisema shule hiyo ambayo ni miongoni mwa zilizochaguliwa kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum ina watoto 41 ambao hulazimika kufundishwa kwenye darasa moja.

**Watoto 41 wenye uhitaji maalum, 15 wana matatizo ya akili, waliobakia ni viziwi, wasioona, wenye ulemavu wa viungo na usonji.**

"Tatizo kubwa lililopo hapa shuleni kwetu ni uhaba wa vyumba vya madarasa na vifaa kwa ajili ya kuwafundisha watoto wenye mahitaji maalum hali inayotulazimu hata wanafunzi wanaofanya vizuri kutoendelea mbele. Tumejaribu kulitenganisha hilo darasa moja kwa kutumia mbao, lakini bado kuna mwingiliano wa kelele na shughuli zingine zinazofanywa na hao watoto," alisema Mwansombelo.

Aliongeza kuwa watoto 41 wenye mahitaji maalum, 15 wana matatizo ya akili, waliobakia ni viziwi, wasioona, wenye ulemavu wa viungo na usonji.

Utaratibu wa elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum, alisema unaruhusu wakifika darasa la tatu kuanza kujichanganya na wenzao kupitia mfumo wa Elimu Jumuishi na kama hawaelewi wanawapima kwa majaribio na kwamba wakibaini hawajaelewa wanakaa nao kuwaelekeza.

Alisema utaratibu huo umesaidia kujenga urafiki nao wako huru kueleza shida zao na kuelewa kwa urahisi.

Alisema kabla ya kuanzishwa kitengo cha kuwahudumia watoto wenye mahitaji maalum, shule ilikuwa ikiwahudumia watoto wa kawaida hivyo miundombinu iliyopo haikidhi mahitaji ya wenye ulemavu.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Jona Kanyeka, alisema kitengo maalum kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalum shuleni hapo kilianza mwaka 2012.

Alisema kuna uhitaji mkubwa wa miundombinu kwa watoto wenye ulemavu, hususani viwanja vya michezo, uzio, vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na madarasa.

Aliongeza kuwa hadi sasa kuna walimu watatu akiwamo mmoja wa kujitolea ambao wanawafundisha watoto hao hitaji likiwa ni walimu sita.

Mwalimu Kanyeka alisema licha ya vikwazo vinavyowakabili shuleni hapo, serikali inatoa Sh. 500,000 hadi 700,000 kila mwezi kwa ajili ya chakula kwa watoto wenye mahitaji maalum.



Mwezeshaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Rehema Mwateba, akiendesha mafunzo ya maandalizi ya ujenzi wa nguvu ya pamoja katika kuimarisha mila na desturi chanya kwenye jamii zinazohusu wasichana kwa washiriki kutoka Kata za Shilela na Lunguya, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Madereva walia ubovu barabara

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya madereva 30 wa magari yanayosafirisha viazi kutoka vijiji mbalimbali vya Kata ya Ilungu wilayani Mbeya, wameiomba serikali kuendelea kuboresha barabara ya Mbeya – Makete kupitia Isyonje ili kurahisisha shughuli za usafirishaji.

Wakizungumza na Nipashe katika Kijiji cha Igoma wakati wakipakia viazi vyao, walisema adha ya barabara kwao imechangia kutumia muda mrefu kusafirisha bidhaa hiyo kutoka shambani hadi kwenye barabara kuu ya Tanzania Malawi.

Mmoja wa madereva hao, Abdallah Juma, alisema kwa sasa barabara hiyo ina mashimo mengi na kwamba kipindi hiki cha kiangazi kinafaa zaidi kuiboresha kabla ya mvua za masika kuanza.

Alisema magari yanayopakia bidhaa hiyo hulazimika kutumia siku 14 hadi 20 kutoka maeneo ya vijiji kwenda mjini kutokana na barabara kutopitika kwa urahisi.

"Tumekaa hapa kwa muda wa wiki moja na siku kama mbili, kitendo cha kukwama hapa kimetuongezea gharama za maisha na hata viazi tulivyobeba kuna hatari vikaharibika tukiwa bado tupo njiani, tunaomba serikali itusaidie kuirekebisha," alisema Juma.

Naye Raphael Mwandembwa, alisema baadhi ya magari yamekuwa yakiharibika kutokana na ubovu wa barabara hiyo na kwamba wanatumia muda mrefu kusafiri kipande kidogo.

Alisema eneo hilo linazalisha viazi kwa wingi kuliko maeneo yote ya Mbeya na serikali inakusanya fedha nyingi kutokana na viazi hivyo, lakini hakuna anayekumbuka kuboresha barabara hiyo.

"Tunamuomba Waziri mwenye dhamana ya miundombinu hii atusaidie maana gari ikiingia kwenye haya mashimo unaweza ukakata hata sipringi, sasa hivi tuna wiki hapa tunahangaika na magari haya na gharama zinaongezeka," alisema Mwandembwa.

# Watakiwa kuwaunga mkono wanawake wenzao

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAWAKE wamehimizwa kuendelea kuwaunga mkono wanawake wenzao walioteuliwa katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kupitia vyama vya siasa kwa kuhakikisha wanawafanyia kampeni na hatimaye kuchaguliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya hali ya kisiasa mkoani Mbeya.

Alisema moja ya mambo ya msingi ambayo yanatakiwa kuzingatiwa ni pamoja na wanawake baina yao kuungana kwa pamoja ili kuweza kushinda nafasi nyingi za uongozi.

Chalamila alisema kuna tabia kwa baadhi ya wanawake kutoaminiana na kuona hawawezi kuwa viongozi na kuona bora kura yake kumpa mwanamume, jambo ambalo halina tija.

Kwa mujibu wa Chalamila, jambo hilo linachangia kurudisha nyuma harakati za wanawake katika kuwasilisha ajenda zao kwenye vyombo vya kutunga sheria.

Alisema hadi sasa Jimbo la Mbeya Mjini na Rungwe ndio pekee walisimamisha wagombea wanawake kugombea nafasi ya ubunge hivyo wanawake wana nafasi ya kushirikiana nao.

"Jengeni tabia ya kupendana na kushirikiana katika kila hali. Wapigieni kura viongozi wote wanawake walioshiriki kwenye kinyang'anyiro cha kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili mjiletee maendeleo," alisema Chalamila.

Hivi karibuni, akiwa mkoani Mbeya, Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi NEC, Asina Omari, alisema lugha za matusi, kejeli na dharau dhidi ya wanawake waliogombea hazitavumuliwa na kwamba atakayebainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

Aliwaomba wananchi kuwaheshimu wagombea wanawake kwa kusikiliza sera zao na Oktoba 28 wakafanye maamuzi ya kupiga kura.

Alisema sheria inaruhusu wagombea wanawake kuwafungulia mashtaka wale wote wanaotoa lugha za matusi na kejeli kwa wagombea hao wawapo majukwaani au maeneo mengine ya kufanyia kampeni.

"Hakuna mtu aliyekuja hapa duniani bila kuzaliwa na mwanamke, hivyo wanawake wanatakiwa kuheshimiwa katika jamii kwa kuwa ndio chachu katika kuweza kuleta maendeleo kwa taifa," alisema Omary.

Miongoni mwa wanawake, akiwamo Mwanaisha Shaban, alisema lugha za udhalilishaji na matusi ni chanzo kikubwa kinachosababisha washindwe kujiamini kwa kuhofia matusi.





# Dk. Mwinyi aahidi kupigania, kuboresha haki za wafanyakazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema akichaguliwa kuwa rais anakusudia kupigania haki za wafanyakazi na kuondosha malalamiko yaliopo ambayo yamekuwa chanzo cha kurudisha nyuma juhudi za ufanisi wa kazi na uwajibikaji na kuwakatisha tamaa.

Dk. Mwinyi alisema hayo juzi alipokutana na Jumuiya ya Vyama vya Wafanyakazi katika ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul Wakil, mjini hapa, ikiwa ni sehemu ya mikutano yake ya kuonana na makundi mbalimbali.

Alisema haiwezekani kupatikana ufanisi wa kazi na mafanikio kama baadhi ya wafanyakazi watakuwa wakilalamika na kudhulumiwa haki zao kwa makusudi.

"Nikichaguliwa kuwa rais, nimejipanga vizuri kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili wafanyakazi wa serikali na watumishi wa umma. Huwezi kupata ufanisi wa kazi na tija kama wako watumishi ambao watakuwa wakikandamizwa na kunyimwa haki zao," alisema.

**Mheshimiwa liko tatizo katika wizara na taasisi zetu. Serikali haitaki kuwasomesha wafanyakazi wake hata pale wakiomba likizo ya masomo wanakataliwa.**

Pia aliwataka wafanyakazi ambao wamekabidhiwa majukumu mbalimbali kuwajibika na kuonyesha thamani ya dhamana waliyopewa, ili kuleta ufanisi wa kazi.

"Haki na wajibu ni watoto mapacha. Nimeyasikia malalamiko yenu, lakini na mimi naomba kura ili niwe rais kwa ajili ya kuyafanyia kazi matatizo yenu," aslisema.

Mapema, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar (ZATUC), Khamis Mwinyi, alisema wafanyakazi wa serikali na sekta mbalimbali ikiwamo isiyo rasmi, wamejenga matumaini makubwa kwa mgombea huyo kwa kuonyesha nia ya utendaji wa kazi na mabadiliko makubwa ya kiuchumi.

Alisema wameshuhudia kwa muda wa mwezi mmoja sasa mgombea huyo amefanikiwa kuyafikia makundi mbalimbali yakiwamo ya vijana, wajasiriamali, kinamama, wazee na wajane kwa ajili ya kusikiliza matatizo na changamoto zinazowakabili.

"Sisi shirikisho la vyama huru vya wafanyakazi ambao tunafanya kazi na taasisi mbalimbali, tumeridhishwa na juhudi unazozichukuwa ikiwamo staili ya kampeni zako kwa kuyafikia makundi mbalimbali ya kijamii ambayo kwa miaka mingi hayajafikiwa na kusikilizwa kero zao," alisema.

Swaumu Othman, mjumbe wa ZATUC, alizitaka wizara na taasisi za serikali kuwasomesha wafanyakazi wake kwa kuwaendeleza kwa lengo la kuleta ufanisi wa kazi.

"Mheshimiwa liko tatizo katika wizara na taasisi zetu. Serikali haitaki kuwasomesha wafanyakazi wake hata pale wakiomba likizo ya masomo wanakataliwa," alisema.



Makamu Mwenyekiti wa Timu ya Ushindi ya ACT- Wazalendo, Mansoor Yusuf Himid, akihamasisha wananchi katika mkutano wa kampeni uliohutubiwa na mgombea wa wa urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad (hayupo pichani), katika viwanja vya Magereza Tomondo, Unguja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ataka wasikubali maneno ya chuki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar, kupitia Chama cha ADC, Hamad Rashid Mohamed, amewataka wananchi Kisiwani Pemba wasikubali kupandikizwa chuki za uchochezi za kufanya fujo kuelekea uchaguzi mkuu Oktoba 28, mwaka huu.

Amesema katika kipindi hiki, wananchi wanapaswa kuepuka viashiria hivyo kwa sababu baada ya uchaguzi, maisha yataendelea kama kawaida.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara Chakechake juzi, Hamad alisema kiko chama kimekuwa na mawazo duni yaliyopitwa na wakati kwamba kisiwa cha Pemba ndiyo ngome yake na hakuna chama chochote chenye uwezo wa kisiasa.

"Wananchi wa kisiwa cha Pemba msikubali kudanganywa kwa kuenezwa sumu na chuki za kisiasa kwa kufanya fujo na kuhatarisha amani na utulivu uliopo. Kisiwa hiki tulitiwa maneno na tukaingia katika vurugu na kusababisha maafa kwa vijana kupoteza maisha, alisema.

Aliwataka wananchi wa Wilaya ya Chakechake kukichagua chama chake ambacho kimejipanga kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi kwa wananchi wa kisiwa hicho ikiwamo kuimarisha kilimo cha karafuu.

Hamad alisema utafiti umefanywa na kuonyesha kwamba katika nchi za Bara Hindi, Kiarabu na Ulaya, liko soko kubwa la mazao ya viungo ambalo halijatumiwa kikamilifu na wakulima.

Naye mgombea mwenza wa nafasi ya urais wa Muungano kupitia chama hicho, Shoka Khamis Juma, aliwataka wananchi wakichague chama hicho ili kutekeleza ilani kwa kufanya mageuzi makubwa ya kiuchumi ikiwamo kujenga viwanda katika ukanda wa maeneo huru ya kiuchumi yaliyoko Micheweni.

"Eneo la Micheweni limetangazwa maeneo huru ya uchumi tangu mwaka 1992, lakini kwa bahati mbaya hadi sasa halijatumiwa kikamilifu katika ujenzi wa viwanda," alisema.

# Rais ajivunia jengo la kisasa biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali imejenga jengo la biashara la Michenzani ili wananchi waingie katika utaratibu wa kuuza biashara kwa njia za kisasa.

Akizungumza katika ufunguzi wa jengo hilo jana, maarufu kama "Michenzani Mall", lililoko mjini hapa, alisema majengo ya biashara kama hayo hayajengwi kwa ajili ya kuuza na kununua vitu peke yake bali yanajumuisha huduma mbalimbali za kijamii kama elimu, afya, urembo na burudani.

Dk. Shein alisema ndani ya jengo hilo, kuna maduka, sehemu za mazoezi ya viungo, sinema, sehemu za kucheza kwa watoto na shughuli kadhaa za kijamii.

Aliongeza kuwa eneo hilo, awali palijaa makontena ya biashara ambayo hayakuwa na mpangilio maalum ndipo serikali ikaamua kuwawekea wananchi mazingira bora ya kuvutia ya kufanya biashara.

Shein alisema sekta ya biashara ina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya uchumi na ustawi wa wananchi na ina uwiano mkubwa na usafiri na usafirishaji ambayo huunganisha watu kutoka vijijini na mijini, kanda, kitaifa na kimataifa.

Alisema serikali anayoiongoza iliivalia njuga kazi ya uimarishaji wa sekta ya ujenzi kwa kuongeza ujenzi wa barabara mpya na kuzifanyia matengenezo zile ambazo zilikuwapo.

Kuhusu historia ya biashara Zanzibar, Dk. Shein alisema katika kujitafutia maisha kabla ya Mapinduzi, wananchi hawakuwa na fursa za kumiliki biashara kubwa kwa sababu biashara za aina hiyo zilihodhiwa na mabepari.

"Majengo kama haya ya biashara tunayakuta katika nchi za wenzetu na yameanza zamani tangu 1922 kule Marekani katika Jiji la Kansas na likiitwa "Country Plaza," alisema Dk. Shein.

Aidha, alisisitiza kwamba wale wote waliokuwa wakifanya biashara katika eneo hilo kabla ya kujengwa jengo hilo, watapewa kipaumbele katika maombi ya kufanya biashara katika eneo hilo kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

Naye Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa, alisema mradi huo ni utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015-2020 juu ya hatua za kuimarisha mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), ili uendelee kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kiuchumi.

Katika miaka 10 ya uongozi wa Dk. Shein, (ZSSF) imewekeza miradi 12 mikubwa pamoja na miradi mengine midogo ambayo yote hiyo imegharimu Sh. bilioni 140.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Khamis Mussa, alisema kuwa baada ya kukamilika kwa michoro mnamo Aprili 30, 2018 ilitolewa zabuni kumtafuta mkandarasi.

Alisema katika mchakato huo, wazabuni 28 walijitokeza na baada ya tathmini Kampuni ya CRJE kutoka China ilishinda zabuni hiyo, hivyo kutiwa saini mkataba wa ujenzi baina ya ZSSF na kampuni hiyo Aprili, 2018 kwa gharama ya Sh. bilioni 27.9.

Alisema kuwa ujenzi ulianza rasmi Novemba 23, 2018 na ulitarajiwa kuchukua miezi 21 hadi kufikia Juni 30, mwaka huu, lakini kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huo ikiwamo kuibuka kwa maradhi ya COVID-19, mradi uliongezewa muda.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Nipashe

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0782253676

Nipashe

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PAULO KIHHEDE KISAVELI** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 887 ADS** aina yake **HONDA-CRV.**

POLISI TAARIFA:

**DOD/KIB/RB/336863/2020.**

115931902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;295/2020**

**Ombi la ELIZABETH PAUL MWAKALOSI, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SIMON MWAKIBIBI MWAKALOSI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 06/10/2020.

Tarehe 6/10/2020

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MOROGORO

115932202

---

**IN THE DISTRICT COURT OF GEITA AT GEITA**

**MISC/CIVIL/APPLICATION CASE NO. 10 OF 2020**

**Emmanuel Paschal Mshanga......................... Applicant**

**Versus**

1. **Ferrant Processing Company Ltd.................. Defendant**
2. **Nyarugusu Mining Co. Ltd**
3. **Borassus Co. Ltd**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT,** the above case has been fixed for hearing/mention on the day of 8 October 2020 at 8.30 A.M in the forenoon.
YOU ARE, required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents on which you intend to rely in support of your case.
**GIVEN UNDER** my hand and SEAL of the Court this 24 day of September 2020.

.........................................
**PRINCIPAL/SENIOR/RESIDENT/MAGISTRATE**

**TO BE SERVED UPON:**
**Ferrant Processing Company ltd**
**C/o Leonard S. Joseph**
**Leonard & Company Ltd Advocate**

**Capn: Point Management District**
**P.o Box 11975**
**Mwanza Tanzania.**

115932302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo ya CHAMWINO MJINI.**

**Usimamizi wa mirathi 88/2020**

**Ombi la SAIDA IDDI LUPOLA kuteuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu IDDI ABDU LUPOLA KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria shauri wakitaka mnamo tarehe 12/10/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe 23/09/2020

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO MJINI
DODOMA.

115932602

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA MBULU (DONGOBESH)**

**SHAURI LA ARDHI NA. 1/2020**

**PASKALINA GENDA .....................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ESTA GITONGE..................MJIBU MAOMBI**

**Mdaiwa ESTA GITONGE, popote ulipo.**

**Fahamu kwamba mleta Maombi PASKALINA GENDA ameleta maombi Na. 1/2020 dhidi yako.**

Hivyo basi kama unakusudia kupinga maombi hayo unatakiwa ulete majibu yako na uwepo Barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria, Shauri limepangwa kutanjwa tarehe 20.10.2020.
Endapo hautatekeleza haya Shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.
Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 23/09/2020.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MBULU

115932702

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GRACE UMBE MWAKITWANGE** amepotelewa kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN CUBE** Namba ya usajili **T 992 BMY,** Iliyotolewa na mamlaka ya mapato Tanzania, yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Taarifa.

POLISI TAARIFA

**DAR/OST/RB/713836/2020**

115931702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;293/2020**

**Ombi la ABEID ABDALLAH NAMKAPE,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SEIF SAID GWAJE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 03/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/10/2020.

Sahihi ya Hakimu

HAKIMU
MOROGORO

115931802

---

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Zitto apata ajali ya gari

**Na Elizabeth Zaya**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe na wenzake watano, jana walipata ajali ya gari katika eneo la Kalya wilayani Uvinza mkoani Kigoma walipokuwa safarini kwenda Lukoma kwa ajili ya kampeni Jimbo la Kigoma Kusini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Ofisa Habari wa chama hicho, Arodia Peter, Zitto alikuwa na watu wengine watano kwenye gari lake.

"Zitto amepata ajali ya gari akiwa njiani kuelekea Lukoma kwenye kampeni katika Jimbo la Kigoma Kusini na alikuwa na watu wengine watano kwenye gari yake na wote wako salama ingawa wamepata majeraha na wanahisi maumivu makali.

"Wamepata huduma ya kwanza palepale katika eneo la ajali na baadaye wamepelekwa Kituo cha Afya Kalya kilichoko Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma," alisema Arodia katika taarifa yake hiyo.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, Martin Otieno, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

"Ni kweli tuko hilo limetokea katika eneo la Kalya, Uvinza, Zitto alikuwa na wenzake watano akiwamo mgombea ubunge wa Jimbo la Kigoma Kusini.

"Tayari timu ya wataalamu imefika kwa ajili ya kuwahudumia na tunaendelea kufanya uchunguzi zaidi wa chanzo cha ajali na tutatoa taarifa zaidi baadaye," aliahidi Kamanda Otieno.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakari Kunenge (katikati), akiwa ameongozana na viongozi wa dini, wakikagua ujenzi unaoendelea wa daraja la Tanzanite, litakalounganisha eneo la Upanga Seaview na Oysterbay, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ofisa Habari ACT kizimbani

**Na Hellen Mwango**

OFISA Habari wa Chama cha ACT-Wazalendo, Doto Rangimoto (34), mkazi wa Tabata Kimanga jijini Dar es Salaam, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na shtaka la kusambaza picha za ngono mtandaoni.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Janeth Mtega, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini jana.

Wakili wa Serikali, Ashura Mzava, alidai mshtakiwa ametenda kosa hilo kati ya Januari Mosi na Februari 26 mwaka huu huko katika eneo la Tabata jijini.

Ilidaiwa kuwa siku hiyo, mshtakiwa Daud alisambaza picha za ngono akitumia simu yake mkononi aina ya Tecno T301 kupitia akaunti ya Twitter yenye jina la James Michael @ James Michae huku akijua kufanya hivyo ni kosa na kinyume cha sheria.

Hata hivyo, mshtakiwa alikana kutenda kosa hilo na aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti aliyopewa likiwamo la kuwa na mdhamini mmoja wa kuaminika na kutakiwa yeye na mdhamini huyo kutia saini bondi ya Sh. milioni tano.

Kwa mujibu wa upande wa mashtaka, upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamlika na kesi hiyo itatajwa Novemba 2 mwaka huu.

# Meneja wa Laizer atimuliwa kikao cha mazishi ya mlinzi

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

FAMILIA ya marehemu Manase William (48), aliyekuwa mlinzi wa bilionea mpya wa madini ya tanzanite, Saniniu Laizer, imewatimua wawakilishi wa Laizer kwenye kikao cha mipango ya mazishi ya mfanyakazi huyo, ikidai kukosa ushirikiano tangu kutokea kwa kifo cha ndugu yao.

Manase alikutwa ameuawa katika lindo lake alfariji ya Septemba 27 mwaka huu na mwili wake ulifanyiwa uchunguzi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru Oktoba 3 mwaka huu.

Uamuzi wa kutowaruhusu wawakilishi wa bilionea huyo kushiriki kikao hicho, ulithibitishwa jana na Mwenyekiti wa Kikao cha Familia hiyo ambaye ni mzee wa ukoo, Godson Osing'a.

Osing'a alisema familia ya mlinzi huyo imeridhia mwili wa marehemu utazikwa Oktoba 10, mwaka huu nyumbani kwao Ilkiding'a wilayani Arumeru mkoani Arusha katika makaburi ya familia.

"Hakuna haja ya kumbembeleza mmiliki wa mgodi msibani kwa ndugu yetu na kama familia hatutoshirikiana na wao. Tangu awali wameshindwa kutoa ushirikiano hata siku ya tukio, Laizer ndiyo alikuwa wa kwanza kufika kwenye tukio akiwa na polisi.

"Laizer kushindwa kufika nyumbani kwa marehemu tangu tukio hilo limetokea ni kuonyesha dharau kwa jamii yetu na hatuhitaji msaada wake katika mazishi ya ndugu yetu," alisema.

Kiongozi huyo wa ukoo wa marehemu Manase aliongeza: "Jana (juzi) tulikubaliana kwamba Laizer atafika kwenye kikao cha leo (jana) ili kulia na wafiwa, lakini badala yake ameshindwa kufika na kuwatuma wawakilishi ambao tuliwakataa. Hii ni dharau kubwa. Kwa hiyo, sisi hatuwahitaji, tutazika wenyewe."

Alipotafutwa kuzungumzia madai ya kufukuzwa katika kikao hicho, mdogo wa bilionea Laizer, aitwaye Yako Laizer, ambaye alimwakilisha kaka yake, alisema wamesikitishwa na hatua ya ndugu wa marehemu kutowapa ushirikiano katika msiba huo.

Yako alisema; "Hata sisi familia ya Laizer tumeumizwa na kifo hicho ila kaka yangu ameshindwa kufika katika msiba huo kwa sababu yupo safarini."

Vilevile, Meneja wa Mgodi wa Bilionea Laizer, Kiria Laizer, alisema kutimuliwa kwao katika kikao hicho na ndugu wa marehemu, kumewasikitisha, lakini akasisitiza kuwa wanajipanga kuhudhuria mazishi ya mlinzi wao na watahakikisha haki na stahiki za marehemu zitapatikana.



# SMALLING SASA JUMLA AS ROMA

**ROME, Italia**

HATIMAYE Chris Smalling amesajiliwa kwa mkataba wa kudumu katika Klabu ya AS Roma ya nchini Italia.

Roma imemsainisha mlinzi huyo kutoka Manchester United kwa mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya pauni milioni 13.6.

Shirikisho la Soka nchini Italia liliandaa stakabadhi ya uhamisho huo dakika moja kabla ya kukamilika kwa dirisha la uhamisho nchini humo.

Smalling mwenye umri wa miaka 30, alihudumu msimu uliopita kwa mkopo katika klabu hiyo na kuisaidia kumaliza katika nafasi ya tano na hivyo basi kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa msimu huu.

United na Roma zilikuwa zimeshindwa kuafikiana kuhusu dau la uhamisho huo, kabla ya kupatana dakika za mwisho kuelekea kufungwa kwa dirisha la usajili.

Smalling mwenyewe hakuwa na mpango wa kurudi Man United kwa madai kwamba, anajisikia furaha zaidi kucheza kwa miamba hao wa Italia.




# Guendouzi asajiliwa Berlin kwa mkopo

**BERLIN, Ujerumani**

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Matteo Guendouzi, amejiunga na klabu ya Hertha Berlin inayoshiriki Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Guendouzi ametua pale Berlin kwa mkopo hadi mwishoni mwa msimu huu, baada ya kutokuwa na namba pale Arsenal.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, hajaichezea Arsenal tangu walipofungwa 2-1 na Brighton Juni mwaka huu ambapo alihusika katika mgogoro na Neal Maupay.

Mchezaji huyo wa Ufaransa alijiunga na Arsenal akitokea Lorient mwaka 2018, baada ya kuanza soka lake katika akademi ya kukuza soka la vijana ya PSG.

Aliwachezea 'Washikabunduki' hao mechi 82, lakini hakuwa kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo msimu huu.



# CAVANI KUIOKOA UNITED

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imemsajili aliyekuwa mshambuliaji wa Paris St Germain, Edinson Cavani, kwa uhamisho huru.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 3, ambaye aliondoka PSG mwishoni mwa Juni baada ya kumaliza mkataba wake, amesaini kandarasi ya mwaka mmoja.

Lakini katika mkataba huo kuna kipengele cha kumwongezea miezi 12 baada ya kumalizika.

Cavani alifunga mabao 341 katika mechi 556, ikiwamo rekodi ya mabao 200 katika mechi 301 akiichezea miamba hiyo ya Ufaransa.

Pia ana mabao 50 aliyofunga katika timu ya Taifa ya Uruguay ambayo ameichezea mechi 116.

Mechi yake ya kwanza akiichezea United inaweza kuwa dhidi ya klabu yake ya zamani PSG kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, itakayopigwa Oktoba 20.

Kutua kwa Cavani pale Old Trafford kunaweza kuisaidia timu hiyo ambayo wikendi iliyopita ilichezea kichapo cha mabao 6-1 kutoka kwa Tottenham Hotspur kwenye Ligi Kuu England.

Wakati huo huo, Man United imekamilisha usajili wa beki wa kushoto wa Brazil na Porto, Alex Telles kwa mkataba wa miaka minne, huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mkataba mwingine mpya.

Beki huyo mwenye umri wa miaka 27, alitua Old Trafford kwa ajili ya kukamilisha uhamisho huo na tayari amekitumikia kikosi cha timu ya Taifa ya Brazil mechi moja pekee.

Dau la pauni milioni 13.6 limetumika kufanya uhamisho wa mchezaji huyo akitokea kwenye Ligi ya Ureno.

"Ni fahari kwangu kujiunga na klabu kama hii. Nahitajika kufanya kazi zaidi, naweza kuahidi kuwa nitajitolea kwa nguvu zangu zote kuhakikisha naisaidia klabu yangu," alisema baada ya kusajiliwa rasmi.

# RAFINHA
## WA BARCA AJIUNGA NA PSG




**PARIS, Ufaransa**

RAFINHA amejiunga na mabingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain kutoka Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alicheza mechi 29 wakati akiwa kwa mkopo kule Celta Vigo msimu uliopita baada ya kushinda mataji manne ya LaLiga pale Camp Nou.

Mkataba wa kiungo huyo ulikuwa unamalizika kipindi cha majira ya joto kijacho na hajapata nafasi ya kucheza chini ya kocha mpya pale Barca, Ronald Koeman msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, Rafinha ni kama Thiago Alcantara aliyesajiliwa hivi karibuni pale Liverpool na alikulia kwenye akademi ya vijana ya miamba hao wa Catalunya na alianza kucheza kikosi cha wakubwa mwaka 2014.

Hakutumika akiwa benchi wakati Barca ikinyanyua taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na akapelekwa kwa mkopo Celta msimu wa 2013-14 na Inter Milan msimu wa 2017-18.

Kikosi hicho cha Thomas Tuchel, tayari kimemwongeza Moise Kean kwa mkopo kutoka Everton na Danilo Pereira akitokea Porto.



## DOUGLAS COSTA AJIUNGA BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

BAYERN Munich imemsajili, Douglas Costa kwa mkopo wa muda mrefu kutoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alichezea Bayern kati ya mwaka 2015 na 2017 na baadaye kuhamia Juve, awali kwa mkopo kabla ya kusaini mkataba wa kudumu.

Costa mwenye umri wa miaka 30, alicheza mechi 103 kwa 'Bianconeri' hao katika mashindano yote, akifunga mabao 10 na kushinda mataji matatu ya Serie A, pamoja na Coppa Italia mwaka 2018.

"Nina furaha kubwa kurudi tena hapa Bayern," alisema akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Nilikuwa na wakati wa kuvutia hapa Munich na mafanikio makubwa na nina uhakika nitayapata tena hapa."

Mkurugenzi wa michezo wa Bayern, Hasan Salihamidzic aliongeza: "Douglas ataimarisha kikosi chetu hasa kwenye winga na ni mchezaji muhimu sana kwetu.

"Sasa tutakuwa na nguvu kubwa hasa kwa uwapo wa Serge Gnabry, Leroy Sane, Kingsley Coman, Jamal Musiala na Douglas.

"Douglas anaijua vizuri sana Bayern na ataimarika haraka sana kwenye kikosi hiki."

Wakati wake wa kwanza kucheza pale Bayern, Costa alishinda mara mbili taji la Bundesliga, DFB-Pokal na DFL Supercup, huku akifunga mabao 14 katika mechi 77.

Amekuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa Bayern ndani ya siku mbili baada ya ujio wa Eric Maxim Choupo-Moting aliyetua kwa uhamisho huru na Marc Roca kutoka Espanyol aliyesajiliwa kwa ada ya euro milioni 15.

# Juve yamtwaa Federico

**TURIN, Italia**

KLABU ya Juventus imemsaini winga wa Italia, Federico Chiesa kutoka Fiorentina kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 54 katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili, Jumatatu usiku.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amejiunga na mabingwa hao wa Italia kwa mkopo wa miaka miwili kabla ya uhamisho wa kudumu.

Chiesa alipitia klabu ya vijana ya Viola kabla ya kupewa mkataba wa kudumu na baadaye kujiunga na Fiorentina ambako alicheza jumla ya mechi 150, huku akiichezea Italia mara 19.

Nyota huyo ambaye anatajwa kama mmoja wa wachezaji wanaokuja juu zaidi, ametua Juventus kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ushambuliaji.

Chiesa sasa ataungana na Paul Dybala, Cristiano Ronaldo na Morata kwenye safu ya ushambuliaji ya kikosi hicho kilichopo chini ya kocha mpya, Andrea Pirlo.

Pirlo alichukua mikoba ya Mauricio Sarri ambaye alifukuzwa baada ya kukaa kwa msimu mmoja tu na 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin.



DON SOKA
MAGA ULAYA




# PARTEY ATINGISHA KWA MSHAHARA ARSENAL

●●●Arteta asema ni kiungo wa aina yake, mwenye nguvu kubwa na uzoefu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya...

**LONDON, England**

ARSENAL hatimaye imeongeza nguvu kwenye safu ya kiungo kwa kufanikiwa kumsajili, Thomas Partey, waliyekuwa wakimwania kwa muda mrefu kutoka Atletico Madrid ya Hispania, usajili huo ukikamilika dakika 32 kabla ya dirisha la kufungwa juzi saa sita usiku.

Partey mwenye umri wa miaka 27, ameigharimu Arsenal pauni milioni 45 katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili Jumatatu na amesaini mkataba wa muda mrefu (miaka minne), huku mshahara wake ukielezwa kuwa ni pauni 260 kwa wiki kwa mujibu wa Daily Mirror.

Dau hilo linamfanya kukaribia anga za Pierre-Emerick Aubameyang na Mesut Ozil ambao katika klabu hiyo wanavuta pauni 350,000 kila mmoja huku Willian akitia kibindoni pauni 220,000.

Katika usajili huyo, Lucas Torreira amekwenda upande mwingine baada ya kukubali kujiunga na Atletico kwa mkopo wa muda mrefu.

Partey mchezaji wa kimataifa wa Ghana kwa muda mrefu amekuwa akiwaniwa na Arsenal na iliripotiwa kwamba walikuwa wakimhitaji kwa ajili ya kuimarisha safu yao ya ulinzi, huku wakimkosa Houssem Aouar wa Lyon ambaye ameamua kubaki klabu hiyo ya Ufaransa. 'Washikabunduki' hao wameripotiwa kwamba waliwasilisha ofa yao siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la usajili na Atletico hawakuwa tayari kumuachia mchezaji huyo.

Lakini mwisho wa siku Atletico hawakuwa na la kufanya zaidi ya kukubaki kumuuza nyota huyo baada ya Arsenal kufika dau hilo lililokuwa likihitajika ili kuvunja mkataba wake.

Partey alikulia kwenye akademi ya kukuza soka ya Atletico baada ya kutua hapo akitokea nyumbani kwao nchini Ghana mwaka 2012.

Baada ya kucheza kwa mkopo kule Real Mallorca na Almeria, akawa na namba ya kudumu pale Atletico na amekuwa mchezaji wa kikosi cha kwanza kwa misimu mitatu iliyopita.

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta akizungumzia usajili wa Partey amesema: "Tumekuwa tukimwangalia Thomas kwa muda mrefu, hivyo sasa tunafuraha kumpata mchezaji mwenye kiwango bora katika kikosi chetu.

"Ni kiungo wa aina yake na mwenye nguvu kubwa. Ataleta uzoefu wake hapa alioupata kwa muda mrefu kule LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Tumeridhishwa na kiwango chake na ubora wake. Ni mchezaji mwenye akili na tunaangalia uwezekano wa kuimarisha zaidi timu yetu."

## KWA UFUPI

**POCHETTINO ATAJWA UNITED**
MAOFISA wa Klabu ya Manchester United wamewasiliana na aliyekuwa Kocha wa Tottenham Hotspurs, Mauricio Pochettino iwapo watamfuta kazi, Ole Gunnar Solskjaer. ***(Star)***

**MAN CITY WAIKATALIA BARCA**
MANCHESTER City imekataa ofa ya dau la pauni milioni 15.4 na marupurupu kutoka kwa Klabu ya Barcelona ili kumnunua beki, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, katika siku ya mwisho ya kufungwa kwa dirisha la uhamisho. ***(Sky Sports)***

**SHAQIRI ABAKI LIVERPOOL**
LIVERPOOL imekataa kumtoa kwa mkopo winga Xherdan Shaqiri mwenye umri wa miaka 28, lakini atauzwa Januari. ***(Goal)***

**STONES AIKATALIA MAN CITY**
MLINZI wa Manchester City na England, John Stones mwenye umri wa miaka 26, alikataa kuondoka kwa mkopo kuelekea Totenham, kwa sababu hakutaka kuiondoa familia yake. ***(Star)***

**PORTO YASHINDWA KWA FELIPE**
KLABU ya FC Porto ilikuwa na nia ya kutaka kumnunua mchezaji wa West Ham na Brazil, Felipe Anderson mwenye umri wa miaka 27, kwa mkopo hadi mwisho wa msimu, lakini imeshindwa. ***(Sky Sports)***

**BARCELONA YAPOTEZA MAPATO**
BARCELONA imepoteza zaidi ya pauni milioni 181 kama mapato kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. ***(Telegraph)***

**TUCHEL ACHUKIZWA PSG**
KOCHA wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel, amechukizwa na kitendo cha klabu hiyo kushindwa kununua wachezaji katika dirisha la uhamisho. ***(Guardian)***

**GRIEZMAN HAMFURAHII KOEMAN**
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 29, hana furaha na Kocha wa Barca, Ronald Koeman, kumchezesha kama mshambuliaji wa kati. ***(Mirror)***

**SMALLING SASA JUMLA ROMA**
ROMA imemsajili jumla beki wa Manchester United, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, kwa pauni milioni 13, ambazo zinaweza kuongezeka na kufikia pauni milioni 18.1. ***(BBC)***

**SHEFFIELD YAKOMAA NA KONGOLO**
KLABU ya Sheffield United bado inawania kumsajili mlinzi wa Huddersfield, Terence Kongolo mwenye umri wa miaka 26 raia wa Uholanzi. ***(Sheffield Star)***

**MKE WA ROMERO AISHUTUMU UTD**
MKE wa golikipa wa Manchester United, Sergio Romero, ameishutumu klabu hiyo ya Old Trafford kwa kuzuia jaribio la Everton kutaka kumsajili mumewe huyo mwenye umri wa miaka 33 raia wa Argentina. ***(Goal)***

**CUISANCE AIBUKIA MARSEILLE**
KIUNGO Michael Cuisance, 21, amejiunga na Marseille kwa mkopo wa muda mrefu akitokea Bayern Munich, ikiwa ni siku tatu baada ya uhamisho wake wa kutua Leeds United kushindikana. ***(BBC)***

**WEST HAM KWA DAWSON**
KLABU ya West Ham ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili mlinzi, Craig Dawson, mwenye umri wa miaka 30, kutoka Watford. ***(Football Insider)***

# KASEJA AMFUNGUA MDOMO BUSWITA

**Na Adam Fungamwango**

HUKU akimfungua mdomo Pius Buswita aliyemfunga na kujizawadia bao hilo mwenyewe, Kipa wa Klabu ya KMC, Juma Kaseja, amekiri Ligi Kuu Bara msimu huu ni ngumu mno na kila timu imejizatiti kupata ushindi popote pale iwe nyumbani ama ugenini.

Kaseja, kipa wa zamani wa Moro United, Simba, Yanga na Taifa Stars alisema hayo baada ya kumalizika kwa mechi Ligi Kuu kati ya KMC aliyokuwa akiichezea dhidi ya Polisi Tanzania na timu yake kuambua kipigo cha bao 1-0 juzi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Kaseja ambaye ndiye alikuwa langoni, alisema kwenye mechi hiyo walijitahidi kila njia kuibuka na ushindi, lakini walifanya kosa moja ambalo liliwagharimu.

"Ligi ni ngumu, ndiyo maana unaona timu zinashinda ugenini kama nyumbani tu, popote timu inashinda mradi iwe vizuri, lakini pia hata pointi zinabanana, hii inaonyesha ugumu, nadhani mechi hii imekwisha, tumefanya kosa tumeadhibiwa, tunaangalia mechi nyingine," alisema kipa huyo.

Lilikuwa bao la dakika ya 88 lililofungwa na Buswita, mchezaji wa zamani wa Mbao FC na Yanga.

Kwa upande wake mchezaji huyo alisema kuwa bao alilofunga ni zawadi yake mwenyewe kwa sababu amelifunga siku ya kuzaliwa kwake.

"Nimefurahi sana, nimelifunga bao hili siku ya kuzaliwa kwangu kwa hiyo hii ni zawadi yangu mwenyewe, lakini nimefurahi kwa kuifunga timu nzuri ya KMC," alisema Buswita.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, amesema lengo lao msimu huu ni kumaliza ndani ya tatu au nne bora.

Kuhusu kushinda ugenini, kiongozi huyo alisema wao hawana ugeni kwenye mkoa wowote kwa sababu Polisi ni taasisi kubwa ambayo ipo nchini kote.

SOKA...




Wachezaji wa timu ya Ballmun (jezi za njano) wakiwania mpira dhidi ya wapinzani wao, River Valley, wakati wa mechi ya Ligi ya Walemavu iliopigwa Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serengeti yaimwagia Taifa Stars mabilioni

**Shufaa Lyimo na Adam Nyangasa**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia mkataba mwingine wa miaka mitatu na Kampuni ya Bia ya Serengeti wenye thamani ya Sh. bilioni tatu kwa ajili ya kuidhamini timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Katika hafla hiyo ya utiaji saini iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam, ilikwenda sambamba na uzinduzi wa jezi mpya ya timu hiyo ya Taifa ambayo inajiandaa kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Burundi Oktoba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mkapa, ambapo jezi ya bluu itakuwa ya nyumbani na njano ikiwa ya ugenini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, baada ya kusaini mkataba na kisha kufanyika kwa uzinduzi huo wa jezi, Rais wa TFF, Wallace Karia, aliishukuru kampuni hiyo kwa kuamua kuongeza mkataba wa kuidhamini timu hiyo na kudai wameanza kufanya mipango kuhakikisha timu hiyo inafika mbali zaidi.

Aidha, Karia aliwataka wadau na kampuni mbalimbali kujitokeza kuiunga mkono Taifa Stars huku akiahidi kuendelea kushirikiana bega kwa bega na wadhamini hao ambao wameonyesha moyo mkubwa wa kuwasaidia.

"Kwa upande wa TFF leo tumefarijika kuona Kampuni ya Bia ya Serengeti imeamua kuidhamini tena timu yetu ya Taifa na katika kipindi chote cha miaka mitatu kilichopita, timu yetu iliweza kufanya mambo makubwa ikiwamo kufuzu kucheza mashindano ya (Afcon) baada ya kukaa miaka 39 bila kushiriki mashindano hayo," alisema Karia.

Karia alisema fedha zilizotolewa ana imani zitawasaidia wachezaji kuweza kufika mbali ikiwa ni pamoja na kushiriki Kombe la Dunia na kueleza kuwa tayari wameanza mikakati hiyo na kuiomba serikali izidi kuiunga mkono timu hiyo, ili kutekeleza maendeleo ya mpira hapa nchini.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, Hassan Abbas, alisema kwa upande wa serikali mwaka huu, wameandaa bajeti maalumu ambayo wamepanga kutoa fungu la kuisaidia timu hiyo, na kuitaka TFF izidi kuwekeza katika timu hiyo kuhakikisha inapata huduma za kutosha.

Alisema wanaishukuru kampuni hiyo kwa kitendo cha kuamua kuongeza mkataba mwingine na kusema kwa sasa hataki kuona timu ya Taifa inatembeza bakuli, na kuahidi kushirikiana nao ikiwa ni pamoja na kusisitiza kampuni zingine ziweze kuisaidia.

Aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi uwanjani kwenda kuisapoti Taifa Stars itakaposhuka dimbani kuumana na timu ya Taifa Burundi, ili kuwapa hamasa wachezaji wetu ambao wanatusaidia kuitangaza nchi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Serengeti, Mark Ocitti, alisema kampuni yao imekuwa mdau mkubwa wa michezo nchini ikiwamo kuwaunganisha Watanzania kuwa kitu kimoja kupitia michezo na kusema wameamua kuidhamini tena timu hiyo kwa kutambua umuhimu wa michezo kwenye uchumi na kijamii.

"Sio tu kuidhamini timu ya Taifa (Taifa Stars), bali kuendeleza na kukuza mpira wa miguu ambao unapendwa na watu wengi duniani hususan kwa timu hii ambayo imepata mafanikio makubwa chini ya udhamini wetu, ambapo ilicheza mashindano makubwa ya Mataifa ya Afrika (Afcon) baada ya kukaa kipindi kirefu bila kushiriki," alisema Ocitti.

## Hitimana aipotezea Namungo kimataifa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Mrundi Thierry Hitimana, ameyapotezea maandalizi ya michuano ya kimataifa kwa muda, wakati huu timu hiyo ikitarajiwa kuiwakilisha nchini kwenye Kombe la Shirikisho Afrika(CAF).

Hitimana amesema kwa sasa nguvu zake zote, ni kutaka kuona timu yake inasimama na kufanya vizuri katika michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema mwenendo wa kikosi cha timu yake katika mechi tano za ligi hiyo walizocheza hadi sasa, unamfanya kutotaka kusikia juu ya michuano hiyo ya kimataifa hadi hapo itakaposimama na kufanya vizuri kwenye ligi hiyo ya ndani.

Alisema kuna timu ambazo wanawakilisha mataifa yao wameshaanza maandalizi hayo, ila kwa upande wake ni tofauti kwa sababu kwa sasa, anafikiria kujenga kikosi chake kufanya vizuri katika ligi ambayo matokeo hayo yatamsaidia kuandaa wachezaji wake kimataifa.

"Kutofanya vizuri katika mechi zetu tatu kwa kukubali kufungwa, ni kwa sababu hatukuwa na maandalizi ya msimu mpya, kikosi changu kilikutana kwa siku saba na kwenda kucheza Ngao ya Jamii baada ya hapo tumeanza ligi kwa hali hiyo sitaweza kupata matokeo mazuri kwenye mechi za mwanzoni mwa ligi hiyo," alisema na kuongeza.

"Kwa sasa sipendi kusikia hizo taarifa za michuano ya Kimataifa, ningekuwa nimeanza vizuri ligi, nina imani kwa muda huu ningetumia jiwe moja kuua ndege wawili, lakini mambo ni tofauti kabisa kwangu, nalazimika nipambane kutengeneza muunganiko wa timu ili kufanya vizuri katika mechi zetu za ligi," alisema Hitimana.

## Pete Muungano kupigwa Tanga

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

CHAMA cha Mpira wa Pete (Netball) Zanzibar (Chaneza) na kile cha mchezo huo kwa upande wa Tanzania Bara (Chaneta), vinatarajia kuandaa Ligi Kuu ya Muungano itakayoanza mwishoni mwa mwezi ujao mkoani Tanga na kushirikisha timu 12 za wanawake na sita za wanaume.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Chaneza, Said Mansab, alisema ligi hiyo inatarajiwa kuanza kutimua vumbi lake Novemba 28 mpaka Desemba 6, mwaka huu.

Alisema kwa upande wa timu hizo 12, sita zitatoka Zanzibar na idadi kama hiyo zikitoka Tanzania Bara huku kwa wanaume nazo zikiwa tatu kwa tatu Bara na Visiwani.

Alizitaji timu za upande wa Zanzibar kwa wanawake kuwa ni KVZ, Mafunzo, JKU, Zimamoto, Chipukizi na Uroa, kwa upande wa timu za Wanaume ni JKU, KVZ na Mkanyageni.

Aidha, alisema kuwa timu zote ambazo zitathibitisha kushiriki ligi hiyo ya Muungano zitapaswa kujihudumia gharama zote hadi ligi hiyo itakapomalizika.

# Michezo

Jumatano Oktoba 7, 2020

Nipashe




## PARTEY ATINGISHA KWA MSHAHARA ARSENAL

HABARI UK 22

## YANGA YAMWACHIA MWAMBUSI SIMBA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umeweka wazi kuwa benchi lao la ufundi litaendelea kubaki chini ya Kocha Msaidizi, Juma Mwambusi, ambaye atakinoa kikosi cha timu hiyo kuelekea mchezo dhidi ya watani wao wa jadi, Simba utakaopigwa Oktoba 18, mwaka huu katika Uwanja wa Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Makamu Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Frederick Mwakalebelea, alisema baada ya kumuondoa Kocha Mkuu, Mserbia Zlatco Krmpotic, timu itakuwa chini ya Mwambusi pamoja na makocha wengine waliokuwapo wakifanya nao kazi.

Alisema wanaendelea na mchakato wa kutafuta kocha ambaye atakuja kurithi nafasi ya Zlatko waliyemuondoa wiki hii baada ya kufikia makubaliano.

"Hadi sasa hakuna kitakachoharibika kwani mipango inakwenda vizuri na kikosi kinaendelea na mazoezi chini ya kocha Mwambusi kuelekea mechi yetu dhidi ya Simba, tumeanza kuangalia namna gani tunaweza kumpata mrithi wa Zlatko," alisema Mwakalebela.

Aliwataka mashabiki na wadau wa timu hiyo wasiwe na mashaka juu ya mchakato wa kupata kocha pamoja na maandalizi yao kuelekea mechi hiyo ya watani wa jadi.

"Kila kitu kinaenda vizuri kuhusu maandalizi yetu kuelekea mchezo huo, pamoja na jinsi gani ya kupata mrithi wa Zlatko kuja mapema nchini ikiwamo kabla ya pambano hilo," alisema Makamu huyo.

## MAWINDONI...



Baadhi ya wachezaji wa Taifa Stars, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam jana, kujiandaa na mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Burundi itakayopigwa uwanjani hapo Jumapili wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SAMATTA AITETEA ASTON VILLA

## ●●●Awaangukia mashabiki Bongo wanaoiponda, akifunguka maisha ya Fenerbahce, mechi na Burundi...

**Na Adam Fungamwango**

HUKU akiwa ameanza vizuri maisha mapya kisoka katika Klabu ya Fenerbahce ya Uturuki, Nahodha wa timu ya Taifa, Taifa Stars, Mbwana Samatta, amewaangukia mashabiki wa soka wa Tanzania wanaoikashifu klabu yake ya Aston Villa kwenye mtandao wake wa kijamii baada ya kuamua kumtoa kwa mkopo kwa Waturuki hao.

Samatta ambaye alitua jijini Dar es Salaam jana alfajiri akitokea Uturuki tayari kwa ajili ya kujiunga na Taifa Stars kuelekea mechi ya kirafiki dhidi ya Burundi Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Mkapa, ameanza vema maisha ya soka Fenerbahce baada ya kuifungia mabao mawili Jumamosi wakati ikishinda 2-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Fatih Karagumruk FC.

Mechi hiyo ilikuwa ya pili kwa Samatta kuichezea Fenerbahce, ikiwa ni baada ya kucheza wakati wakitoka sare tasa dhidi ya Galatasaray.

Akizungumza baada ya kuwasili nchini, Samatta alisema maneno ya 'shombo' ya baadhi ya Watanzania wanayoyaandika kwenye mtandao wa kijamii wa Aston Villa kwa kuizodoa timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya England aliyokuwa akiichezea, yanaweza kusababisha vijana wengine wa Kitanzania kushindwa kuchukuliwa kucheza si tu Aston Villa bali hata kwa timu nyingine kubwa nchini humo na kwingine Ulaya.

"Mimi naona tu waache, kwanza watawatia ugumu Watanzania wengine, ukiondoa mimi. Mimi naweza kurudi au kutorudi, lakini kuna vijana wengi wanacheza mpira wa miguu na Aston Villa wanaweza kuvutiwa nao, lakini wakikumbuka kuwa ni Mtanzania na kilichotokea huko nyuma, wanaweza kunyimwa bahati ya kujiunga nao, kikubwa waache na wawe na subira tu, kikubwa ni subira," alisema straika huyo wa zamani wa African Lyon, Simba (za Tanzania), TP Mazembe (DR Congo) na Genk ya Ubelgiji.

Hata hivyo, Samatta alisema ni kweli kuna mengi yamepita nyuma ya pazia hadi kufikia uamuzi wa kwenda Fenerbahce, lakini kwa sasa hawezi kuyaweka hadharani kwa sababu bado anacheza soka.

"Kuna mengi yamejitokeza hadi mimi kufikia uamuzi wa kuhama, lakini sidhani kama ni wakati sahihi kwa sasa kuyazungumza, bado naendelea kucheza soka si jambo zuri kuyasema, lakini nikimaliza soka langu na kustaafu, nitatafuta utaratibu wa kuyasema yote niliyoyapitia kwenye maisha ya soka," alisema Samatta.

Akizungumzia maisha yake mapya ndani ya Fenerbahce, alisema: "Timu mpya, watu wapya, lugha mpya, kila kitu ni kipya, lakini mambo yatakwenda sawa tu nitazoea."

Kwa upande wa kikosi kilichoitwa Stars, Samatta alisema na mechi inayowakabili dhidi ya Burundi, Samatta alisema ana imani wanaweza kufanya vizuri Jumapili.

"Nimeona majina yaliyoitwa na ligi ilikuwa inaendelea, hivyo ninaamini tunaweza kufanya vizuri," alisema nahodha huyo wa Stars.

Baadhi ya mashabiki wa soka nchini ambao walijiunga kwa wingi kwenye mitandao ya kijamii ya Aston Villa, baada ya Samatta kujiunga na klabu hiyo Januari mwaka huu, nao wamekuwa wakiiacha, huku baadhi wakitoa maneno ambayo yanaonekana ni kama kuishutumu klabu hiyo kwa kile wanachokiona kuwa ni sawa na kutomtendea haki nohodha huyo wa Stars, kutomlinda au kumsaidia ili afanye vema kwenye ligi hiyo pendwa na badala yake kumtoa kwa mkopo kwenye klabu hiyo ya Uturuki huku kukiwa na kipengele cha kuruhusiwa kumnunua jumla.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002